Mwenendo Wa Nabii Wa Kweli Wa Mungu

Lo, habari za asubuhi marafiki. Ni asubuhi nzuri, na wakati unaofaa kuwa hapa. Nina furaha kuwa mzima asubuhi ya leo, na kuwa hapa pamoja na kusanyiko hili tena. Kuna mambo mengi sana yanayoweza kutukia katika muda mfupi jinsi hii. Wala hatujui ni wakati gani tutakapoitwa, kujibu, huko juu kwenye Mahakama kuu. Nasi tunataka kuwa tayari wakati wowote, ili tupate kuwa na amani.

2 Nami nina shukrani sana, kama nilivyosema. Hakika, nilikuwa hapa Jumapili usiku, nami nilikuwa nikiwazungumzia watu. . .Nilihubiri Jumapili usiku, na ninataka kumshukuru Ndugu Roberson, ninyi nyote mliopiga simu, kuhusu kufurahia huo Ujumbe wa Jumapili usiku, "Tuna vitu yote." Na kwa hiyo mimi. . .Wakati fulani sikuwazia nilikuwa nitazungumza, nilikuja tu huku nikamwangalia Ndugu Neville. Koo la—lake ni kama la nyuki avumaye kule chini. Nikawazia, "Maskini ndugu, hakika kama akinipigia simu usiku wa leo, nitasaidia, ama nifanye kila niwezalo." Maana, ninajua hilo ni nini, wakati umechoka na kupwelewa na sauti, na alikuwa amehubiri sana asubuhi hiyo. Na kwa hiyo ni—nilihubiri kwa niaba yake Jumapili usiku. Na kwa hiyo tuna—tuna. . . Ninawashukuru, sana.

3 Sasa kuna maombi mengi, wanasema, kwa ajili ya maombi. Na kwa hiyo hebu na tayakumbuke tu, kwanza, maombi haya yote. Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

4 Baba yetu wa Mbinguni, imeandikwa ya kwamba tunapaswa kuingia kwenye kusanyiko Lako tukiwa na shukrani mioyoni mwetu, kuyafanya maombi yetu yajulikane katika makusanyiko ya Watakatifu. Nasi tunayo mengi, asubuhi ya leo, mengi sana, hata hatujui jinsi ya kukuelezea, bali Wewe unayajua. Kuna mengi ambayo hayakutajwa. Unayajua, pia. Kwa hiyo, tunaomba kwa mioyo yetu yote, kama tulivyofanya Jumapili iliyopita usiku kwa ajili ya nanii wa Dada Shepherd, mtoto, wa Ndugu Shepherd. Hapo wakati tukiwa katika ninii. . .Kurudi, Roho Mtakatifu alisema, "Hana polio yoyote. Atapona." Ni ridhaa ya jinsi gani tuliyo nayo tunaposikia kutoka Kwako.

5 Sasa tunaomba asubuhi ya leo ya kwamba utatujalia maombi haya kwa ajili ya wagonjwa, kwa nyumba ya waliofiwa, kwa wapendwa, na yote ambayo yamekwisha kunenwa, Baba. Tunaomba ya kwamba utamkumbuka kila mmoja. Basi ninatoa maombi yangu, na maombi ya watu hawa, mbele Zako;

yamekusanywa pamoja, na yanatumwa Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Tusikie, Baba, tunaomba. Amina.

6 Ninataka kumshukuru kila mmoja wenu ninyi nyote kwa maombi yenu kwa ajili yangu. Wakati mimi . . . Mnajua nilikuwa na mlipuko mdogo huko kwenye mahali pa kulenga shabaha kule chini. Na Shetani alijaribu kuniua. Na—na, hakika, asingeweza kufanya hivyo. A-ha. La. Mungu hakuwa amemaliza nami bado. Kwa hiyo hawezi kamwe kufanya hivyo mpaka yote yamekwisha. Mungu atakapomaliza, basi niko tayari. Lakini mimi . . . Rafiki yangu wa kweli, Ndugu Woods, kule chini, ni rehema tu za Mungu, la sivyo angekuta tu kutoka *hapa* kwenda chini, bali si kutoka *hapa* kwenda juu. Ulikuwa mlipuko wa tani tano ama sita uliokuwa karibu *hivi* na uso wangu, namna *hiyo*. Haukunidhuru hata kidogo. Unaona? Ulikwaruza uso wangu kidogo. Kwa hiyo, hilo, vema, yote yamekwisha sasa, ni alama moja ndogo tu iliyosalia *hapo*.

7 Kwa hiyo, ninataka kuwashukuru Ndugu na Dada Dauch hapa. Ndugu Brown, na hao wengine, ambao walifahamu kwa mazungumzo ya simu hata wakakusanyika pamoja, kundi la watu, na kuniombea. Na hilo kweli ni jambo fulani, linakufanyia jambo fulani. Unajua, unawaombea wengine, na kila kitu, na basi unapokuta kwamba mtu fulani anakuombea wakati unapoyahitaji, hilo linamaanisha jambo kubwa sana. Na ninajua wengi wenu hamkuja, ama chochote kile, bali mliniombea haidhuru. Na hilo linamaanisha jambo kubwa sana kwetu. Na hiyo ndiyo sababu ambayo mimi . . . halikunidhuru. Mungu aliniacha kuwa mzima. Na kwa hiyo ninashukuru sana.

8 Sasa, nina matangazo kadhaa kabla tu ya kuwaweka wakfu jamaa hawa wadogo. Sasa, usiku wa leo, kuna ibada maskanini. Na ninyi nyote mnaokuja hapa maskanini, njoni moja kwa moja kwenye ibada hapa. Na kwa hiyo tunaninii . . . Ninaenda kuzungumza kwa niaba ya Ndugu Ruddell, usiku wa leo, hapa nje kwenye barabara kuu, mmoja wa ndugu zetu waliotutembelea. Halafu basi, mara nitakaporudi, kama nina usiku mwingine, ninataka kwenda kwa Ndugu Junie Jackson. Halafu yule ndugu kule Sellersburg, tunamwia usiku mmoja pale, na kwa hiyo tunataka tupande twende kule kumwona. Na yule ndugu kule Utica, tukiingia kwenye siku hizi usiku tuwezavyo.

9 Juma hili ninaondoka kwenda Green Bay, Wisconsin, kama mjuavyo, kwenye mkutano wa maeneo ya Wafanyabiashara wa Full Gospel.

10 Jumapili ijayo, niko kwenye shule ile ya sekondari ya juu, iliyoko kule juu, nilikokuwa mara ya mwisho kule. Ninasahau jina la ukumbi huo wa shule hiyo ya sekondari ya juu. [Ndugu fulani anasema, "Mather."—Mh.] Yaitwaje? ["Mather."] Mather.

Stephen Mather. Naam. Vema. Ukumbi wa shule ya sekondari ya juu.

11 Halafu basi, Jumatatu, niko kwenye mkutano huko mahali nilikokuwa na mahojiano na lile shirika la wahudumu kule Chicago, mara ya mwisho kule. Tuko mahali hapo kwa ajili ya mkutano wa kumuaga Ndugu Joseph Boze, ambaye anaenda Tanganyika. Tanganyika, ninaamini ndivyo anavyoiita. Na Kenya, na Durban, na kupitia kule, akifanya maandalizi kwa ajili ya mikutano yangu ijayo ya majira ya majani kupukutika; na huko Afrika, na kupitia Afrika Kusini. Na basi tunawaomba mtukumbuke kwa maombi katika mikutano hii. Kisha tutarudi.

12 Wala sijui ambapo nina wakati wa kupata, siku nyingine maskanini, ama sina, kabla hatujaenda basi mpaka huko Carolina ya Kaskazini. Na halafu, kutoka huko, twende Carolina ya Kusini. Halafu kotekote mpaka Cow Palace huko Los Angeles, kule South Gate. Na huko ndiko ninakotarajia kwenda nikamwone Bw. Weatherby, yule aliyeitengeneza ile bunduki ambayo risasi yake ililipuka.

13 Hakuagiza nafasi ya kichwani irudishwe nyuma mno, na kuifanya risasi isukume nyuma badala ya kwenda mbele. Ilikuwa ni bunduki ya zamani ambayo nilimpelekea tu. Aliagiza itobolewe, wakati huo, na kuifanya bunduki ya aina nyingine. Nilitia risasi ndani yake, nikaiinua nitupe risasi, nayo, vema, ililipua bunduki hiyo yadi hamsini kunizunguka, namna hiyo, ikayeyukia mkononi mwangu. Mtutu ulitupwa kwenye ule mstari wa yadi hamsini, bolti ikaenda moja kwa moja nyuma ya tundu la kulungu, yadi thelathini, arobaini nyuma yangu, na vipande vya marisau vikaruka na vikakwang'ua maganda kwenye miti na chochote kile. Kwa hiyo hiyo ilikuwa karibu *hivi* na jicho langu, karibu tu inchi moja, mahali ilipolipukia namna hiyo. Na kama ingalikuwa imelipua . . .

14 Na bunduki hiyo itastahimili presha ya ratili elfu sita mia tisa, yenyewe, bila kulipuka. Kwa hiyo mnaweza kuwazia kulikuwa na kiasi gani juu yake, kufanya hivyo. Pia kumbukeni, kama italipua hiyo, ingaliweza kulipua kichwa changu na mabega pia, unaona. Lakini alikuwepo Bwana amesimama pale, ambaye hakuruhusu hata inidhuru, ilinikwaruza tu kwenye uso. Na marisau madogo yaliingia chini ya upande mmoja wa jicho langu, yakafanya duara kuzunguka jicho, kwa hiyo hayakudhuru jicho, ambapo marisau yalipenya. Kimoja cha vipande vikubwa vilivyochoma fuvu la kichwa kililizunguka jicho, hakikuingia kwenye jicho, hata hivyo. Loo, jamani!

15 Si muda mrefu uliopita, mnakumbuka, niliwaambia ya kwamba Yeye alinikuta chumbani, na akasema, "Usiogope, kwa maana uwepo usioshindwa wa Yesu Kristo uko pamoja nawe milele." Unaona? Unaona? Kwa hiyo hilo linathibitisha jambo hilo, ya kwamba Yeye yuko.

16 Daktari aliyeangalia jicho langu huko Louisville, alisema walimwandikia Dk. Sam Adair hapa chini, rafiki yetu, na kusema, "Jambo pekee ninaloweza kusema, ni kwamba Bwana alikuwa ameketi pale asubuhi hiyo pamoja na mtumishi Wake apate kumlinda, la sivyo hata asingekuwa na kichwa na mabega yaliyosalia." Kwa hiyo, Yeye alikuwa mwema sana kwangu, nami ninathamini jambo hilo. Linanileta karibu zaidi. Daima linaleta tofauti kidogo.

17 Na halafu, siku mbili baadaye, siku tatu, baada ya kuwa nikienda kwenye mkutano wangu, ambao nilikuwa nimepangiwa huko Canada, mtu huyo, bila kujua lolote kuhusu jambo hili, alinipigia simu, na ilibidi aahirishe mkutano huo. Unaona? Ningalikuwa njiani nikienda huko, kama jambo hili lisingalikuwa limetukia namna hiyo. Unaona? Na kwa hiyo basi akapiga simu tena, nami inanibidi kuchukua mkutano huo, mkutano wa Canada. Na hiyo itakuwa ni kwenye Julai, majuma ya mwisho ya Julai. Kisha nitaendelea na safari hadi Dawson Creek, halafu kwenda hadi Anchorage, Alaska, Bwana akipenda.

18 Sasa, hakuna mmoja wa mikutano hii ambapo nina mwongozo wowote wa kwenda huko, hata mmoja. Lakini siwezi kuwazia juu ya kuketi hapa msimu wote wa kiangazi, kuketi huku, na watu wakifa kila mahali. Sina budi kupanda mbegu, popote pale, haidhuru nini. Kama hazitamea, kama ndege wa angani wakizipata, chochote kile, ninataka kupanda mbegu, maana Yeye alinipa baadhi yake kuzipanda. Kwa hiyo ni—nitaipanda hiyo Mbegu kwa vyovyote vile. Sasa, tuna wakati hapa ambapo mimi . . .

19 Watu wengi, wanachoita, "kubatiza" watoto wachanga katika imani ya Kikristo. Vema, hilo ni sawa, kama ukifanya hivyo. Hiyo ni juu yako. Bila shaka, kwa kweli hawawabatizi. Wananyunyiza tu maji juu yao. Lakini, kwangu mimi, ninapenda kudumu tu na yale Biblia iliyosema tufanye. Kwa hiyo, vile tu Neno lilivyosema, hivyo ndivyo ninavyotaka kufanya, vile tu Hiyo ilivyosema. Na, sasa, si—sipati mahali popote katika Biblia . . .

20 Katika Agano la Kale, waliwaleta watoto kwa tohara ya kimwili, watoto wa kiume, naye mama akatoa sadaka kwa ajili ya utakaso, hua wawili ama mwana-kondoo.

21 Lakini, katika Agano Jipya, mahali pekee ninapoweza kupata kumbukumbu la ibada hii kuu ya . . . Ilikuwa ni kuwekwa wakfu. Waliwaleta watoto wachanga kwa Yesu, Naye akawachukua mikononi Mwake na kuwabariki. Hivyo ndivyo wazazi walivyofanya wa siku Zake. Na maisha Yake yalikuwa ni mfano wa vile tunavyopaswa kufanya. Unaona? Mambo haya aliyafanya kwa kutoa mfano.

22 Sasa, tunawachukua tu watoto wachanga, nao wanawaleta kwetu, nasi tunawainua juu tu kwa Mungu, na kuomba baraka za Mungu juu yao, na kuomba ombi la kuwekwa wakfu kutoka kwa mama na baba, kwa Mungu, wanapomtoa mtoto wao. Na. . .ama kuwaweka wakfu katika Jina la Yesu Kristo, mpaka watakapokuwa wenye umri wa kutosha kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Na sasa, Yeye alisema, "Lolote tufanyalo kwa neno ama kwa tendo, tufanye yote katika Jina la Yesu Kristo." Kwa hiyo—kwa hiyo hivyo ndivyo tunavyotaka kufanya.

23 Na sasa, wakati dada akicheza polepole wimbo huu mdogo, dada, tunao hapa, *Waingizeni*. Na akina mama na akina baba walio na watoto hawa wadogo ambao hawajapata kuwekwa wakfu kwa Bwana, kama mtawaleta sasa, wakati kusanyiko, tunapowaimbia polepole sasa, wimbo. Naam.

Waingizeni, waingizeni,
Waleteni watoto wadogo kwa Yesu.

24 Nawapenda jamaa hawa wadogo. Kuna jambo fulani kuwahusu ambalo ni tamu sana.

25 Nadhani huyu kweli ni Mwitaliano. Sivyo? Vema. Familia ya Kiitaliano, wachache ambao wanapaswa kuwekwa wakfu. Dada mdogo Mwitaliano kutoka, loo, kutoka Chicago, yupo hapa. Kasema, "Hii ni familia ya Kiitaliano, asubuhi ya leo, bali sitahubiri."

26 Jina Lake ni nani? Jonathan David, ni jina zuri jinsi gani! Sasa, Jonathan. Alisema baba yake alikuwa na—alikuwa na jina la Kiitaliano, naye alikuwa. . .Anataka mtoto wake mchanga aitwe kwa jina la Biblia.

27 Mwajua, kulikuwako na Mwitaliano mashuhuri katika Biblia, jina lake Kornelio, wakati mmoja, mwajua. Alikuwa na kikosi, naye alikuwa mkarimu, na aliwapa watu sadaka, wakati yeye akiwa ni Mmataifa, bado. Mnajua hadithi hiyo. Na siku moja Malaika alikuja nyumbani kwake, akamwambia atume kumwita mtu aliyejua mpango wa Mungu. Na yeye. . . Mnajua hadithi hiyo. Wakati, aliwafanya watu hao wamheshimu sana Mungu! "Petro alipokuwa akisema Maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia." Hiyo ni kweli. Ninaomba ya kwamba mtoto huyu mchanga atakuwa mtu wa namna iyo hiyo, jina lilo hilo.

28 Jonathan, mzuri! Ninaweza kumshika? Njoo hapa, Jonathan. Jamani, ni bonge dogo la jinsi gani la sukari kwa familia hii!

Na tuinamishe vichwa vyetu.

29 Baba yetu wa Mbinguni, miaka imepita, kama hadithi hii ambayo ndiyo kwanza niinukuu, ya mtu mashuhuri jina lake Kornelio, ambaye alikuwa ni mtu mkarimu, mwenye haki, akitoa sadaka na kumpenda Mungu. Ndipo Malaika wa Mungu akaja nyumbani kwa mtu huyo. Ee Mungu, tunakupa Wewe, asubuhi

ya leo, mtoto Jonathan David. Naomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba kama vile nilivyomchukua kutoka kwenye mikono ya mama na baba yake, ambao wanamtoa Kwako . . . Ninaomba ombi hili la kuwekwa wakfu kwa maisha ya mtoto huyu kwa ajili ya maisha ya utumishi Kwako, baraka kwa nyumba yao, jiwe kuu la kuvukia kwa Kanisa. Tujalie, Baba. Ninakupa Wewe mtoto Jonathan David, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

30 Mungu na awape neema Yake na msaada wa kumlea katika maonyo ya Mungu.

Ubarikiwe, Jonathan David.

31 Sasa, huyu, jamani, ni mvulana mdogo kweli, ama ni msichana? Mvulana? Jamani, mhubiri mwingine anayekuja, natumaini. Jina ni nani? Mika. Mika. Ninazungumza juu yake asubuhi ya leo. Mika Edward. Edward, hilo ni jina zuri. Sasa, mke wangu angeweza kufanya hivi vizuri zaidi inapofikia kumshika, maana daima mimi ninaogopa nitawavunja wakati wakiwa ni wachanga. Unaona? Ni kitoto kitamu jinsi gani, hayo macho madogo yakiangalia tu kote. Yeye ni mdogo sana. Ana umri gani? Umri wa mwezi mmoja.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

32 Baba wa Mbinguni, hawa mume na mke vijana wanakuja hapa tena kukutolea matokeo ya muungano wao wa maisha uliyowapa, kumlea katika maonyo ya Mungu. Mbariki huyu Mika mchanga. Mungu, naomba ya kwamba utamfanya mtu kama Mika katika Biblia. Tujalie, Baba. Mpe baraka za Mungu. Mbariki baba yake na mama yake, na umfanye mfano wa kuvutia hapa duniani, jiwe kuu la kuvukia kwa ajili ya huduma ya Kristo. Na sasa, tusikie, Baba, ninakutolea, kutoka mikononi mwa baba na mama, ninamweka katika mikono ya Mungu, mtoto Mika Edward, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

33 Bwana na ambariki, awabariki, baba na mama, kumlea katika maonyo ya Mungu.

Ninaamini hakuna wengine. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

34 Loo, ninawapenda tu hao jamaa wadogo, kila mmoja tu. Kwamba, kila mmoja, ndiye mtoto mchanga aliye mzuri sana ulimwenguni. Kamwe hakuna haja . . . Nilipomleta mtoto Joseph nyumbani, huyo alikuwa, kusema kweli, jamaa mwenye sura mbaya sana niliyepata kuona, bali mimi na mama yake tulifikiri alikuwa ni mzuri sana. Lakini hivyo ndivyo ilivyo, unajua. Hiyo ni . . . Tunafikiri hivyo tu.

35 Sijui, asubuhi ya leo, baadhi ya washiriki wetu hapa. Kulikuwa na ni—ninii . . . Sasa, jicho *hili* lina beladona ndani yake, ambayo inatia kiwi sana. Lakini Dada Nash . . . Kauliza habari za Ndugu Nash; sijui kama alikuwa amepata nafuu.

Yu. . . Wako hapa? Loo, vema, naam, yupo hapa. Bwana asifiwe, Ndugu Nash. Hilo, hilo ni zuri.

36 Sasa, Dada Edwards, je! yupo hapa? Ninii. . . Ama, Dada Shepherd, aliyekuwa na yule msichana mdogo, mgonjwa, je! amepona sasa? Sawa. Nilipata habari hizo, na jambo hilo lilikuwa kama tu dakika tano kabla sijawa na watu, kutoka nje ya mji, kwa ajili ya mazungumzo ya faragha. Nilikimbia chumbani na kuomba, nao walisema mtoto huyo alikuwa anapatwa na polio, mikono na miguu ilikuwa ikikakamaa. Ndipo nikaingia upesi kuomba, na kusema, "Nitakuja baada ya ibada." Nikamwambia Loyce apige simu na kumwambia mama huyo ya kwamba nitakuwa kule baada ya ibada; kama alinihitaji, anipigie simu. Ndipo nilipoingia kuomba, Roho alisema—alisema, "Hakuna polio. Atakuwa mzima." Nikashuka nikaja, vema, sote tulifanya maombi hapa kanisani. Hilo lilitosha kabisa.

37 [Dada fulani anasema, "Ndugu Branham?"—Mh.] Naam, mama. [Tulienda kwa daktari Jumatatu, baada ya wewe kumwombea mara ya kwanza, na pleurisi yote kifuani mwake imekwisha, imeondoka kooni mwake."] Bwana asifiwe! Maombi hubadilisha mambo.

Aisee, yeye hayupo hapa, asubuhi ya leo, yupo, yule mkwe? Naam.

38 Jumapili iliyopita, mara ya mwisho niliyohubiri hapa, Jumapili ya Juma lililopita, kulikuwa na jamaa mdogo aliyeketi hapa; nilikaza kumwangalia. Nikawaza, "Ninapaswa kumjua jamaa yule." Ndipo nikaja kujua kwamba, alikuwa ni mwana wa mwenzi wangu shuleni, Jim Poole. Mbona, tulikua pamoja, tangu tulipokuwa wavulana wadogo, tukikua. Yeye ndiye niliyekuwa naye kwenye ile ajali ya bunduki, wakati ule, na baadaye alikuwa na nyingine mwenyewe, na rafiki yangu. Ninaamini ya kwamba ninaweza kumwongoza mvulana huyo kwa Kristo. Nilimjaribu baba yake kwa bidii sana. Ninaamini nitafaulu, bado, nitamwingiza. Natumaini ninaweza kumwongoza jamaa huyo mdogo. Alikuwa na ninii. . . Nilimwangalia kwa kila namna. Alionekana kana kwamba alikuwa na ninii mzuri, kile ninachoita sasa (msimwambie mtu mwingine yeyote tamshi hili), lakini, mtetemo wa roho yake, hisi nzuri. Ninaamini haitachukua jitihada kubwa mno kumwongoza mvulana huyo kwa Kristo. Kwa hiyo na tumwombee. Hiyo ni kweli.

39 Na, ndugu, unaona, mtu mwingine alikuwa ni mgonjwa, ama jambo fulani, ambalo ninajaribu kuwazia.

40 Hata hivyo, tunawaombea wote. Na wakati mara nyingine. . . Unapotuma ombi, kumbuka, mara ninapolipata. . . Mke wangu yumo jengoni mahali fulani, nadhani, kwa hiyo yeye anajua. Mara ninapopata ombi, moja kwa moja ninaingia kwenye chumba changu cha kusomea, ninaingia kwenye

maombi, na kukaa mle mpaka nitakaposikia kitu fulani. Kamwe sikati tamaa.

41 Hivi majuzi, wakati Sam, Dk. Sam, alipotoa vitu hivyo kwenye jicho langu, alikuwa akijaribu kuvitoa, na lilimtia uchungu sana, ilimbidi kuweka taulo juu ya uso wangu. Kasema, "Siwezi kuangalia damu ya rafiki yangu msiri." Kasema... Nami nilikuwa nimelowa hiyo, mwajua. Akasema—akasema, "Siwezi kabisa kufanya hivyo na kushughulika katika hiyo." Unaona? Na kwa hiyo akaitoa hiyo. Na kesho yake alikuwa hospitalini. Kwa hiyo nikamwombea, naye akatoka akiwa mzima.

42 Na ndipo siku ya pili, mke wake, hata hawakujua alikuwa na shida gani, walifikiri alikuwa akishikwa na polio. Unaona? Kasema, na akasema...Nami nikamwombea, na sasa yuko nyumbani akiwa mzima. Kwa hiyo tukaingia chumbani, Dak... Tukaingia ofisini, na yeye...Tukafunga mlango pamoja, kasema, "Sasa, Ndugu Bill, nitakuomba jambo fulani." Kasema, "Je! utaniombea mimi na Betty?"

Nikasema, "Hebu. Hebu na tuombe."

43 Kwa hiyo, huyo ndiye ambaye Bwana alionyesha lile ono, mahali pa kujenga kliniki. Ninyi, mnakumbuka hadithi hiyo. Kama mkiitilia shaka, pitieni kule mkamwulize siku moja. Naam, ndiyo kwanza aseme, "Hebu mtu yeyote na aje tu." Kasema, "Nimewasimulia watu elfu kumi jambo hilo."

44 [Ndugu mmoja anasema, "Ndugu Branham?"—Mh.] Naam, ndugu. ["Kwa wale walio hapa asubuhi ya leo na ili kuweka imani zaidi ndani ya mioyo ya wengine: Jumapili asubuhi ya Pasaka, ulimwita mtu wa thamani hapa, wa tatu, ambaye alikuwa ni mwanamume. Ulisema alitoka Seymour. Nawe ulisema, kwa upako wa Roho Mtakatifu, 'Wanakuita, "Bill."' Ninamjua mtu huyo. Ninamjua vizuri sana. Na baada ya sisi kuondoka hapa, jina lake ni Isaka. Kweli wanamwita 'Bill'"] Ndiyo, bwana. Unaona?

45 Jina lake halisi ni Isaka. [Huyo ndugu anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Bali wanamwita Bill. ["Hiyo ni kweli."]

46 Roho Mtakatifu hakosei. Yeye hawezi kukosea. Sasa, hii, mtu fulani alikuwa akizungumza, kasema... "Mimi—mimi nina umri wa miaka hamsini na mitatu, na tatu, karibu miaka thelathini na moja, nimekuwa nyuma ya mimbara, nami nimemwona katika makumi ya maelfu ya mambo."

47 Jana, nilikuwa huko chini, chini kabisa, kusini mwa Kentucky, moja kwa moja kwenye mpaka wa Tennessee, nami nilikuwa nimeketi kwenye mashua pamoja na Ndugu Daulton, ambaye Bwana alimpa watoto wake wote. Mnakumbuka ile asubuhi hapa, wakati alipoanza kutoka. Naye akasema, "Ndugu Branham," kasema, "nadhani ingekuwa ni vigumu kwako kukadiria."

48 Nikasema, “Loo, Ndugu Daulton, makumi elfu mara makumi elfu ya mambo kama hayo.”

Kasema, “Kwa nini usijaribu kuandika kitabu” (Nikasema . . .) “cha jambo hilo?”

49 Nikasema, “Loo, jamani, Ndugu Daulton, kinge—kingepita mashua hii hapa, ensaiklopidia, majuzuu tu ya vitabu vya yale nimemwona Bwana akifanya. Wala hakuna wakati mmoja Yeye ameshindwa, unaona, si hata wakati mmoja; lakini, kamilifu kila wakati.”

50 Naona, ninaamini sasa, kama sikosei, msichana wa Ndugu Shepherd, akiwa amevaa nguo ya namna fulani yenye rangi ya chungwa. Ndivyo ninavyofikiri. Nilisimama karibu naye, hivi majuzi asubuhi. Alikuwa akitembea akienda kule chini, nami nikafikiri huenda nikambeba msichana mwingine, kwa hiyo nikaondoka. Kwa hiyo huyo aliyesimama alikuwa ni mimi, dada. Ni—nilifikiri ilikuwa ni binti wa Ndugu Shepherd, nami ningembeba, maana nilifikiri pengine gari lake huenda liliharibika ama chochote kile. Tulikuwa tukienda, kumchukua Becky. Nami nikadhani huenda ingekuwa ni msichana mwingine. Lakini sasa nimemwona ameketi pamoja nao pale, kwa hiyo ni—ninaamini ilikuwa ndiye msichana yule. Kwa hiyo huyo alikuwa ni mimi niliyekuja kwa gari karibu na pale na kisha nikaondoka.

51 Kwa hiyo, je! kila mtu anampenda Bwana Yesu? Loo, ajabu sana! Hilo ni zuri tu na ni jema sana. Amina.

52 [Ndugu Neville anasema, “Ndugu Willard ndio kwanza aingie.”—Mh.] Vema, Ndugu Willard, tunafurahi tu kuwa nawe humu. Nawe unaonekana uko mzuri sana, pia, vizuri sana ninavyoweza kukuona. Sote wawili kwa namna fulani tumefura kabisa kama sambusa, usoni. Ninaonekana kana kwamba nimepigwa na konzi moja la hiyo. Nami nilimwona Ndugu Willard usiku huo, wakati alipokuwa amelala, na kwa kweli, alionekana anatisha. Lakini unaonekana mzuri sana asubuhi ya leo. Nasi tunampa Mungu shukrani na kumsifu kwa jambo hilo, ndugu. Amina. Naam. Mwajua, ibilisi hawezi kutuua mpaka Mungu aseme, “Njoo.” Ndipo tunataka kwenda, sivyo, Ndugu Willard? Hiyo ni kweli. Mpaka wakati huo yeye anajaribu tu bure. Hivyo tu. Bwana Yesu ndiye msaada wetu na kimbilio letu.

53 Sasa hapa mimi ninazungumza hapa, wakati nina kama saa sita za kuhubiri asubuhi ya leo. Unaona? Ninii tu . . . Sasa, hatukutangaza, hatukutuma tiketi zozote, na kadhalika, maana tayari nilitangaza nisingekuwa hapa. Lakini, kushuka tu kuja huku kumsaidia Ndugu Neville, na nipate kuwaona ninyi nyote tena, na kuwa na wakati kidogo wa ushirika.

54 Na Jumapili iliyopita usiku, Ndugu Roy Roberson, sijui kama yupo hapa ndani, ama hayupo. Siwezi kuona vizuri kutambua

kama yupo hapa. Alinipigia simu, alikuwa akiniambia juu ya ule Ujumbe.

55 Na mtu fulani alipiga simu, akasema, “Nilikuwa nikishangaa wakati ulipozungumza juu ya ‘Mungu alitupa vitu vyote.’” Unaona? Alitupa. Alitupa uzima. Hebu jaribu kuununua. Alitupa upendo. Jaribu kuununua. Alitupa furaha. Jaribu kuinunua. Alitupa amani. Jaribu kuinunua. Hakuna njia ya kuinunua. Huwezi kuinunua.

Ndipo nikasema, “Alitupa mauti.”

Mtu fulani akapiga simu, akasema, “Mhubiri, nilishangaa mahali ulipokuwa ukielekea na jambo hilo.” Kasema, “Nilifikiri, ‘Loo—loo, hapa Ndugu Branham alijifunga wakati huo.’” Si wakati Biblia inaposema hivyo. Unaona? Biblia ilisema Yeye alitupa mauti.”

56 Sasa, tunaweza kufanya nini na mauti? Unajua, Paulo alipokaribia mauti, alisema, “Ee mauti, u wapi mwiba wako?” Mauti haitutawali. Tunaitawala. Kweli. Mambo yote tumepewa sisi.

57 Na halafu nilitoa mfano wa jinsi ambavyo kwamba Israeli, walipokuwa wakienda kwenye nchi ya ahadi, hawakuwa wameiona nchi hiyo kamwe. Hawakujua lolote kuihusu. Walikuwa tu na ahadi ya Mungu, kulikuwako na nchi, nayo ilikuwa imejaa maziwa na asali, na ni nzuri, na—na ni mahali pa kupendeza sana. Na ilikuwa . . . Kamwe hawakuwa wameiona. Hakuna mtu aliyepata kuwako huko, aliyejua lolote kuihusu. Bali walikuwa wameahidiwa hiyo. Na kwa imani wakasafiri wakaingia jangwani.

58 Na wakati walipofika mpakani kabisa, walikuwa na shujaa pale jina lake ni *Yoshua*, ambalo linamaanisha, “Yehova Mwokozi.” Kwa hiyo alivuka Yordani, akaingia kwenye nchi ya ahadi, na akaja na ushahidi ya kwamba nchi hiyo ilikuwa iko. Ninapenda jambo hilo. Nayo ilikuwa ni nchi nzuri. Watu wawili walibeba kichala kimoja cha zabibu kutoka huko. Ilikuwa ni nchi nzuri, kwa hiyo alirudi na thibitisho ya kwamba nchi waliyokuwa wakienda kuimiliki ilikuwa iko.

59 Sasa, kwa Kanisa, tunasafiri kwenda katika Nchi ya wasiopatikana na mauti, Nchi ambamo hamna kufa, Nchi ambamo wafu wanafufuliwa. Nasi tulikuwa na Mwokozi mkuu katika kambi yetu. *Yesu* maana yake ni “Yehova Mwokozi,” Mpendwa. Naye alivuka Yordani ya mauti, akaingia katika Nchi hiyo nyingine, kisha akarudi, na kuleta ushuhuda ya kwamba tunaishi baada ya kifo. Amina. Kwa hiyo kifo kiko wapi?

60 Kisha akatupa vitu vyote. “Sasa tuna amana ya urithi wetu. Kwa jinsi . . . ” Sasa sikilizeni kwa makini. Nami sihubiri juu ya somo hilo, bali linasikika zuri kwangu sasa hivi. Unaona? Hivyo, tuna amana ya huo. Kwa kuwa, siku moja tulitembea katika dhambi; na baada ya kubatizwa katika Jina Lake, na kufufuka

pamoja Naye katika ufufuo, tumetolewa dhambini, hatutataka kamwe tena kurudi mara nyingine. Unaona? Tumefufuliwa kutoka dhambini, pamoja na thibitisho tulilo nalo. Kwa uwezekano tuko katika ufufuo kutoka katika mauti yote. Mnaona? Kama tungeweza kufufuka kutoka dhambini, kwa imani katika Yeye; na kuna dhambi, ni nani angetaka kurudi kwenye kopo la takataka la dhambi tena? Unaona? Tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Unaona? Na hiyo ndiyo amana. Amina. Hiyo ni amana ya ufufuo mkamilifu. Mauti yote, kimwili na kiroho, tayari tumeshinda mauti ya kiroho, maana tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani.

61 Na kama vile Eliya alivyoshuka kwenda Yordani siku moja, na akaupiga, akiwa pamoja na Elisha, na ukarudi ukatengana, naye akavuka. Alirudi akiwa na sehemu maradufu.

62 Nasi tukiupiga Yordani, pamoja na Kristo, tuna sehemu moja, bali tukirudi, tunarudi tukiwa na sehemu mbili. Tuna Uzima wa Milele, kufufuka kutoka dhambini, sasa, katika haki pamoja na Roho Mtakatifu. Na halafu tukirudi, pamoja na Kristo, tunarudi tukiwa pia na ufufuo wa mwili, na tayari tuna ufufuo wa kiroho. Tuna sehemu yake maradufu. Daima mfano wa Kristo na Kanisa: Elisha na Eliya.

63 Loo, sitaki kulianza hilo. Jamani, jamani, jamani, tusingeweza kamwe kuufikia huu Ujumbe wa saa sita hapa. [Ndugu Neville anasema, "Nyama ingali kwenye mfupa, bado."—Mh.] Ndiyo. Jamani! "Nyama kwenye mfupa," Ndugu Neville. Tungali tunaiguguna. Loo, hivi hamna furaha? [Kusanyiko linasema, "Amina."] Unaona? Hatuna . . .

64 Hakuna kusumbuka tena. Mauti si kitu. Tunaimiliki. Ni yetu. Haiwezi kunitawala. Ninaitawala. Jinsi gani? Kwa Yeye aliyenifanya mshindi, kwa maana tayari nimeshinda mauti. Nilifanyaje jambo hilo? Kwa kumwamini Yeye. Unaona? Mauti imo ndani ya dhambi, kutokuamini. Mimi si asiyeamini. Mimi ni mwaminio. Nimefufuka kutoka kwenye kitu hicho, nikafufuliwa. Ni amana ya ufufuo wangu wote mkamilifu wa kimwili, kiroho, kila kitu. Naam, bwana. Mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kwa hiyo tunaitawala mauti, kwa Yesu Kristo Ambaye ameshinda mauti, kuzimu, kaburi, maradhi, huzuni, chochote kile, akashinda yote.

65 Na sisi sasa tumefufuka pamoja Naye, tumeketi katika ulimwengu wa Roho, tukinena kiroho, katika Kristo Yesu, vitu vyote vikiwa chini ya miguu yetu. Hata ufufuo wa kimwili uko chini ya miguu yetu, maana tuko ndani ya Kristo. Mna—mnalipata? Kama mnalipata, inueni mikono yenu. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Amina. Hilo ni zuri. Mradi tu mnalipata, hilo linapendeza. Unaona? Msiachilie . . . Sasa endeleeni tu kuliweka niani mwenu. Unaona? "Tumetoka mautini kuingia Uzimani," kimwili, kiroho, kila njia.

66 Na kila kitu, na mambo yote, ni yetu sasa. Lo, ulimwengu hapa nje unasema sisi ni wenda wazimu, na hata hivyo dunia nzima ni yetu. Utairithije?

67 Wakati, kama nilivyosema, Ibrahimu, unaona, alikuwa kwenye nchi ya ahadi; Mungu alimpa hiyo. Lutu alitekwa na maharamia mahaini fulani, akachukuliwa. Huyo alikuwa ni mpwa wake. Vema. Kila kitu kilichokuwa kwenye nchi ile kilikuwa ni cha Ibrahimu. Pia, yeye hakuwa ni mtu wa vita. Kamwe hakupigana. Hakuwa na wanajeshi wowote. Alikuwa na watumishi. Lakini wakati alipoona kwamba kitu fulani, ibilisi, alikuwa amekuja na kumwibia kitu ambacho kilikuwa ni ahadi kwake, aliwapa watumishi wake silaha naye akachukua silaha. Hakujua jinsi angeweza kulishinda jeshi hili lote la wafalme. Watumishi wachache tu, bali Mungu alimwambia jinsi ya kufanya jambo hilo. Alijigawanya, na kuwapiga wale wafalme, kisha akarudi akiwa mshindi. Kwa nini? Aliweka imani yake juu ya ahadi ya Mungu kwamba kila kitu katika nchi hiyo kilikuwa ni chake, naye Lutu alikuwa ni sehemu yake, hiyo ni kweli, alikuwa ni sehemu ya nchi hiyo. Loo, jamani!

68 Na hapo alikutana na Melkizedeki, baada ya vita kwisha. Je! ungeweza tu kuona Ibrahimu akipanda kuja njiani? Hakujua ya kwamba alikuwa shujaa, bali wakati huo alijua. Naam, bwana. Naye alikutana na Mtu aliyetoa hiyo ahadi, Melkizedeki.

69 Sasa hebu na tusome kutoka katika Kitabu cha Amosi. Nitazungumza asubuhi ya leo; si saa sita, lakini. Natumaini sivyo. Unaona? Kwenye ninii—kwenye somo, kama, *Mwenendo Wa Nabii Wa Kweli*. Na usiku wa leo, Bwana akipenda, nitazungumza juu ya, *Kutoa Presha*, na kwa hiyo Bwa—Bwana akipenda.

70 Sasa, ninajulikana kuwa mkosoaji, lakini mi—mi—mimi si mkosoaji, ila tu kwa jambo lolote baya. Bali mimi, sisi, tunapaswa kukosoa kilicho kibaya.

71 Sasa, kama mtafungulia vinasasauti vyenu sasa, chumbani, mbona, ni sawa. Ninataka kusoma sasa kutoka Amosi, mlango wa 3. Ama ninii . . . Naam. Mlango wa 3 wa Amosi, sehemu yake tu, Amosi 3.

> *Lisikieni Neno hili alilolisema* B*WANA* *juu yenu, enyi wana wa Israeli, juu ya jamaa yote niliowapandisha kutoka nchi ya Misri, nikisema,*
>
> *Ni ninyi tu niliowajua katika jamaa zote zilizo duniani; kwa sababu hiyo nitawapatiliza* . . . uovu *wenu.*
>
> *Je! watu wawili waweza kutembea pamoja, wasipokuwa wamepatana?*
>
> *Simba atanguruma mwituni, asipokuwa na mawindo? Mwana-simba atalia pangoni mwake, ikiwa hakupata kitu?*

Je! ndege ataanguka mtegoni juu ya nchi, mahali asipotegewa tanzi? Mtego utafyatuka juu ya nchi, bila kunasa kitu chochote?

Je! tarumbeta itapigwa mjini, watu wasiogope? Mji utapatikana na hali mbaya, asiyoileta BWANA?

Hakika Bwana. . .hatafanya neno lolote, bila kuwafunulia *watumishi wake manabii* siri *zake.*

Simba amenguruma, ni nani asiogope? Bwana MUNGU amenena, ni nani awezaye neno ila kutabiri?

72 Hapana budi macho yake yalifinyaa, alipokuwa amesimama asubuhi hiyo juu ya kilima ng'ambo tu ya mji wa Samaria. Ninaweza kuona mikono yake thabiti ilipokuwa ikizipapasa ndevu zake zenye mvi. Jua kali lilikuwa likiwaka usoni pa nchi. Hakuwa na madoido apate kuangaliwa. Yuko tofauti jinsi gani na wainjilisti wa siku hizi! Nguo Zake zilikuwa zimejikunjakunja; ndevu zake za matimutimu. Naye akaangalia chini kwenye jiji hilo la Samaria, macho yake yalifinyaa alipokuwa akiangalia. Hakuvutia macho, bali alikuwa na BWANA ASEMA HIVI kwa taifa hilo.

73 Ilikuwa, labda, tofauti sana kwa uamsho huu unaokuja, ambao Bwana amemtuma aende Samaria, kuliko vile wainjilisti wetu wa siku hizi wangekuwa. Hakuwa amejiandaa kwa ajili ya ufufuo kama huo, kama ambavyo tungedhani anapaswa kuwa leo. Lakini kumbukeni, yeye hakuwa mwinjilisti wa kisasa. Alikuwa ni nabii. Hakujali kuhusu zana za kisasa. Yeye alikuwa na BWANA ASEMA HIVI.

74 Hakujali jinsi alivyoonekana, na jinsi gani alivyovalia kimtindo, kama nywele zake zilikuwa zimechanwa vizuri, ama kama mtu yeyote alimwangalia ama hakumwangalia. Yeye alikuwa na Neno la Bwana. Hilo lilikuwa ndilo lengo lake kamili: kuleta Neno hilo la Bwana. Jamaa huyu alikuwa ni nani? Naam. Alikuwa ni Amosi, nabii, mshamba, bali alijua mahali alipokuwa amesimama. Alijua alilokuwa akifanya. Alikuwa ni nabii wa kweli wa Neno. Na sababu ya yeye kuja kwenye jiji hili, ilikuwa ni kwa sababu Neno lilikuwa limemjia.

75 Na wakati Neno la Bwana linapomjia mtumishi wa kweli, hana budi kwenda, haidhuru hali ya mambo ikoje, ama haidhuru kuna shida gani. Hana budi kwenda, kwa vyovyote vile. Kama yeye yuko tayari, kama anajisikia kwenda, kama anataka kwenda, kama chochote kile; hana budi kwenda, haidhuru. Ni Mungu anayenena, naye hana budi kuubeba Ujumbe huu. Kwa sababu, ni . . . Haendei upuuzi. Haendi kwa ajili ya kupata fedha. Haendi kwa ajili ya kupendwa na watu. Yeye huenda tu katika Jina la Bwana, kwa ajili ya jambo moja. Ana hu—huduma, naye ametumwa na Bwana. Naye ni Neno la Mungu, kwa sababu anabeba Neno la Bwana. Huyo ni nabii wa kweli wa Bwana.

Somo langu ni: *Mwenendo* Wa *Nabii Wa Kweli Wa Mungu.*

76 Mtu huyu mashuhuri, mjasiri wa Mungu, alitabiri katika siku za Yeroboamu wa pili. Nina sehemu ya historia yake imeandikwa hapa mbele yangu. Alitabiri karibu miaka kumi na mitatu ya uamsho wake. Na Yeroboamu, alikuwa Yeroboamu wa pili, alikuwa mtu mwerevu na hodari kama wale Israeli ilikuwa nao kwa muda fulani. Alikuwa mtu ambaye alikuwa ameleta usitawi kwa Israeli. Israeli ilikuwa ikistawi. Lakini, yeye, alikuwa na kasoro fulani. Alikuwa ni mwabudu sanamu.

77 Nami kwa namna fulani nilipokuwa nikisoma jambo hili, hivi majuzi, kwa namna fulani nilifikiri hilo lililingana vizuri sana na siku hizi. Haidhuru mtu ni mwerevu jinsi gani, na kiasi gani yale anayoweza kufanya, na usitawi kiasi gani, kama akimwacha Mungu, yeye anawiwa na taifa, mbali na Mungu na Neno Lake. Sijui kama haliendani na sisi, siku hizi, kwa mtu anayependa kuketi kwenye televisheni na kuonyesha jinsi walivyo werevu, kwamba wana akili jinsi gani. Lakini sijui kama wana ya kutosha kuchukua BWANA ASEMA HIVI. Yeye alikuwa mtu mwerevu, vyema.

78 Israeli ilikuwa katika hali ya kurudi nyuma. Wahubiri wake, makasisi wake, na pia serikali yake, wote walikuwa wameliacha Neno la Bwana. Sasa, hawakuamini jambo hilo. Waliamini ya kwamba walikuwa na Neno la Bwana. "Lakini ipo njia inayoonekana sawa kwa mtu, bali mwisho wake ni njia za mauti." Kwa nini walikuwa wamekosea? Kwa nini mtu angeamini hilo—hilo—hilo kama walikuwa wamekosea? Ukasisi mzima wa wanadamu, maelfu ya wahubiri na makuhani, na wafalme na magavana, wote waliokiri kuwa wamwabuduo Mungu, na, hata hivyo, wote walikuwa wamekosea.

79 Halafu, hawakuhitaji mfalme kwa ajili ya usitawi. Walichohitaji ni nabii, kwa sababu Neno la Bwana, ama fasiri ya Neno la Bwana, humjia nabii wa kweli. Wakati mwingine unaweza kuona njia yake ni ipi basi. Ni njia iparuzayo kabisa, wakati makasisi wote, na wahubiri wote, na—na—na waaguzi wote, na—na serikali yenyewe dhidi yake. Lakini, hata hivyo, Neno la Bwana humjia nabii, na huyo peke yake. Yeye ana Neno halisi. Ingawa alikuwa na Biblia ile ile waliyokuwa nayo, bali Neno lilikuja kwake. Mungu alikuwa akithibitisha ya kwamba alikuwa na Neno.

80 Walikuwa na majengo yaliyo makubwa sana na mifumo ya kidini, na kadhalika, waliyopata kuwa nayo, madhabahu yamejengwa kila mahali, na—na kila namna ya—ya mambo, bali hata hivyo walikuwa maili milioni moja kutoka kwenye Neno la Mungu.

81 Nafikiri, mimi mwenyewe, picha hiyo ingelingana vizuri sana na leo, ninaposoma Kitabu hiki cha Amosi. Inawalazimu kukisoma mtakapofika nyumbani. Serikali yote, makuhani, wote walikuwa wameliacha Neno la Mungu.

82 Ningependa tu kusoma sehemu nyingine ya Maandiko hapa, niliyo nayo, kuonyesha ambapo walikuwa wamefanya jambo hilo. Sasa hebu na tusome mlango wa 2 na kifungu cha 4, kwa dakika moja.

> *Haya ndiyo asemayo Bwana; kwa makosa matatu ya Yuda, naam, kwa manne, sitaizuia adhabu yake isimpate; kwa sababu wameikataa sheria ya Bwana;. . .*

83 Hilo ni Neno, walilipuuza, na hata hivyo walidhani walikuwa Nalo.

> *. . .wala hawakuzishika amri* zangu*; na maneno yao ya uongo* yamewakosesha*,. . .*

84 Sasa, wao walikuwa na Neno, Biblia, bali maneno yao ya uongo waliyokuwa wameingiza kwenye Hilo yalikuwa yamewakosesha.

> *. . .ambayo. . .baba zao waliyafuata.*

85 Unaona sababu yake? Sasa, walikuwa wamekosea kwa sababu walikuwa wameweka tafsiri ama mafafanuzi yao wenyewe kwenye Neno. Nami niliona ilikuwa inaendana na siku hizi, kwa kuwa wengi sana wanataka kuweka wazo lao wenyewe kwenye Neno, nasi tunaingia katika machafuko. Ni kemeo jinsi gani kutoka kwa Mungu, alilokuwa nalo nabii huyu.

86 Sasa, Amosi alikuwa nabii wa Mungu, nabii wa kweli. Mtu yeyote ambaye husoma kumhusu Amosi anajua ujasiri wa mtu huyo jasiri wa Mungu. Anahesabiwa kuwa mmoja wa manabii wadogo, maana hakukaa muda mrefu sana, bali hakika aliweka shoka kwenye shina la mti. Alikuwa mmoja wa manabii wajasiri sana, naye alikuja na upako. Alikuja na BWANA ASEMA HIVI. Alijua aliyokuwa akizungumzia, kwa sababu upako wa Mungu ulikuwa juu yake kuwaletea tafsiri ya kweli kwa Neno la Mungu.

87 Amosi alitoka mashambani, nyikani, akaingia jiji lenye ulimbwende. Hakuwa ameshakuwa humo kabla ya hapo. Alikuwa mvulana mshamba, huko mbali sana nyikani. Alipokuwa huko nyuma katika maombi, Mungu alikuwa amekutana naye, na alikuwa amemwambia juu ya uovu wa taifa hili lenye ulimbwende ambalo alikuwa ni sehemu yake. Na Samaria ulikuwa ndio makao makuu, mmoja wa miji mikuu wakati huo, na wa utawala wa Yeroboamu.

88 Na wakati aliposimama pale asubuhi hiyo, kwenye kilele cha kilima, akitembea huku amevaa nguo zake chakavu, chafu za mashambani, labda mavumbi na matope miguuni mwake, na mahali alipokuwa amelala katika vazi hilo chakavu, usiku baada ya usiku. Nami sijui, hakuwa na bafu siku hizo. Huenda ilikuwa ni siku chache tangu alipooga. Lakini hilo halidhuru ndani ya mtu. Muda mwingi sana, siku, kuuvalisha mwili, wala hamna cha kutosha ndani. Tunashughulika sana kuhusu kama tunaoga kila siku, na nywele zetu zimechanwa, na kubadilisha nguo

zetu, na kila kitu, na halafu tunaachilia upande wa ndani uwe vyovyote, tunavaa mavazi yale yale ya dhambi ya siku nyingi, tukiifanya nafsi inuke kwa kanuni za imani na mafundisho ya sharti, wala hatuchunguzi na kuiosha katika Neno la maji ya utengano, kutokana na mambo ya ulimwengu.

89 Aliposimama asubuhi hiyo, akiangalia upande wa pili wa kilima, kwenye hilo jiji lenye mambo ya fahari, uliojaa vitu vya kisasa ambavyo hakuwa amewahi kuviota kwamba kulikuwepo na kitu kama hicho. Israeli ilikuwa katika upeo wake. Ilikuwa na muungano na mataifa yote jirani. Wenye fahari kwelikweli, wanawake wamevaa nadhifu kwelikweli, na wa—wanaume. Nao walikuwa wamezama katika anasa, mashindano ya mbio, na olimpiki, na kila kitu kikiendelea. Si ajabu macho yake yalifinyaa; si kwa madoido ya jiji hilo, kama vile mtalii angefanya, akija New York, ama Los Angeles, akiwaona wanawake walio nusu uchi, wanaume wakifanya yasiyofaa, na dhambi.

90 Marafiki zangu fulani, siku chache zilizopita, walikuwa wakija kutoka kwenye safari ya kuvua samaki, chini tu ya chuo cha Biblia cha chuo mashuhuri cha Biblia, kinachojulikana sana. Na pale, walikuwako wasichana wadogo, wamelala barabarani, kwenye majani, nusu uchi, na wavulana wadogo, labda ni wanafunzi kutoka kwenye chuo hicho, wakinywa pombe na kufanya yasiyofaa, ni chukizo sana.

91 Sasa, kufanya mambo mabaya kama hayo huchochea tamaa ya Wamarekani wengi wanaojiita Wakristo. Wanapoangalia Los Angeles, ama nimewaangalia nikiwa kwenye ndege tunapoingia Los Angeles; hawajapata kuwa huko hapo kabla; ama Hollywood, ama—ama Florida pamoja na taa zao zote za neoni juu ya mi—mitende. Loo, wangepaka pua yao poda upya, na kutengeneza vipodozi vyao. Walifikiri kilikuwa ndicho kitu cha ulimbwende sana walichopata kuona. Na kuona waliochana vizuri na kuvaa nadhifu, wakitembea mitaani, walitaka kutoka waende kule waone ni jinsi gani wanavyoweza kuvaa nguo zilizowabana, ama kujinengua huku na huko mitaani. Ambapo, wanafikiri ya kwamba hilo ni jambo zuri sana.

92 Lakini macho hayo ya nabii huyo yaliyotiwa mafuta na Mungu hayakufinyaa kwa sababu ya huo uzuri, kama vile ilivyo kwa baadhi ya watalii, bali juu ya utovu wa uadilifu, kwa watu walioitwa kuwa wabarikiwa wa Mungu. Macho yake hayakuangalia huo uzuri. Hayakufinyaa kwa sababu ya huo uzuri. Ilikuwa ni kwa sababu ya ta—ta—tabia mbaya na uozo wa watu waliokuwa wameitwa kuwa wateule wa Mungu, na wangefanya mambo kama hayo. Si ajabu, yeye alisema, "Simba ananguruma, ni nani asiogope? Mungu alinena, na ni nani awezaye kujizuia kutabiri?"

93 Aliona upotovu, uozo. Hayo ndiyo aliyokuwa akiangalia. Hapo ndipo alipoona mambo hayo yote. Hayakumvutia. Yaliichefua nafsi yake. Kwa nini? Yeye alikuwa ni nabii. Alijua yale Mungu aliyokuwa ameahidi kubariki, na kwamba baraka ilikuwa ni nini, na jinsi watu wanavyofanya na baraka. Na ibilisi amepotosha katika siku yake, kutoka kwenye baraka halisi ilivyokuwa, kufikia kwenye u—u—uozo wa uadilifu; baraka ya kuvutia macho na tamaa ya watu wasioongoka, kufikia kwenye mapenzi na njia ya Mungu, na njia ya Mungu ya maisha.

94 Jinsi lilivyo mfano kwa siku hizi! Jinsi ambavyo wahubiri wanaweza kusimama mimbarani, na waangalie dhambi na upotovu wa ulimwengu huu, na kuona watu wanaotenda na kufanya jinsi wanavyofanya, halafu wanawabariki tu kwa sababu wao ni wafuasi wa kanisa lao, ama dhehebu, ni zaidi ya jinsi nafsi yangu inavyoweza kuelewa.

95 Mungu anapozungumza, tabiri! Kama Roho wa Mungu akimgusa nabii wa kweli wa Mungu, yeye atapiga kelele kwa Neno hilo. Sitaki kuwa mkosoaji, bali ni nani anayeweza kunyamaza? Ni nani anayeweza kustahimili na kuangalia jambo kama hilo, na kukiri kuwa ni mtumishi wa Kristo, na asilikemee? Sijali kile dhehebu lingesema, ama kile kanisa lolote lingesema; hiyo ndiyo sababu mimi si mfuasi wao. Wangekufukuza, jambo la kwanza. Lakini Neno la Mungu huja kwanza. Kama wewe ni mjumbe, una jambo fulani la kusema. Kama ukisema jambo lolote kinyume na Neno Hili, wewe si mjumbe kutoka kwa Mungu; wewe ni mjumbe wa agano la dhehebu fulani ama wa nadharia fulani. Lakini mjumbe wa Mungu ana Neno la Mungu.

96 Na rafiki yetu, asubuhi ya leo, tulipomwangalia, alikuwa na Neno la Mungu, kwa maana alikuwa ni nabii wa kweli wa Bwana.

97 Sasa, walidhani walikuwa na u—ufafanuzi wake, na wakawaza, "Vema, hakika, angalia yale tunayofanya."

98 Sasa, jambo lenyewe ni kwamba, tunaye amesimama pale juu ya kilima asubuhi ya leo, akiangalia huko, kote chini kwenye jiji hilo. Akitikisa kichwa chake, akiangalia; macho yake yakifinyaa. Akichukua mkono wa vazi lake na kupangusa jasho lake kutoka usoni mwake, na mavumbi. Jua kali likipiga kichwa chake chenye upara. Ndevu zake zikining'inia chini; anazipangusa kwa mikono yake. Yeye hakuona uzuri. Aliona dhambi. Haikumpendeza. Ilimchukiza.

99 Kwa nini yeye asiseme, "Mimi, Mwisraeli, angalia jinsi nchi yangu imesitawi"? Angesemaje hayo wakati akiwa nabii wa kweli wa Mungu, akijua matokeo, na yale ambayo yalikuwa yanaenda kukipata kitu kama hicho?

100 Hebu tumsimamishe juu ya kilima leo na hebu tumwache aangalie chini. Hebu auangalie Jeffersonville, watu wanaojiita Wakristo. Hebu atafute mahali popote Marekani watu

wanaojiita Wakristo. Macho yake yaliyotiwa mafuta na Mungu yangefinyaa tena. Mikono yake ingevuta-vuta ndevu zake. Kwa nini? Yeye haoni uzuri na usitawi ambao ulimwengu unaona. Anaona kule ku—kumwacha Mungu. Anaona utovu wa uadilifu wa watu. Anaona kurudi nyuma kwa taifa. Anaona uozo kanisani. Angefanyaje ila kufinyaza macho yake, na kutamani kuingia mle, kusudi aweze kuurarua vipande-vipande?

101 Vipi kama askofu fulani angalimkuta kule juu, na kusema, "Sasa, je! wewe ndiwe nabii wa Bwana? Sasa, tutakwambia yale unayoweza kusema na yale usiyoruhusiwa kusema." Unafikiri angelisikiliza? Vipi kama wangalisema, "Njoo ujiunge na madhehebu yetu sasa, nasi tutakusaidia katika uamsho wako?" Unafikiri angesikiliza? La. Nisingewazia jambo hilo, kutoka kwa mtu kama huyo. La.

102 Yeye alitumwa na Mungu. Haikumbidi kupata ushirikiano wao. Alikuwa na Neno la Mungu, upako wa Mungu, wakati uliokusudiwa na Mungu. Alikuwa akija katika BWANA ASEMA HIVI. A-ha. Huyo ndiye nabii wa kweli. Hivyo ndivyo anavyosafiri. Hasafiri na lolote ila BWANA ASEMA HIVI.

103 Je! jiji hili la Samaria lenye ulimbwende, Waisraeli hawa wa kimtindo, wenye elimu ya juu, wahubiri hawa na makuhani walioadibishwa vilivyo, wangeweza kumpokea maskini jamaa huyu asiyejulikana? Labda sarufi yake ilikuwa mbaya sana. Alitoka kwenye familia maskini iliyoko nyikani. Aliondoka nyumbani, akaitwa na Mungu, kwenda nyikani kujifunza Mungu na Neno Lake, na akawa nabii. Mungu alimzaa jinsi hiyo.

104 Manabii huzaliwa, mjumbe wa wakati huo, ambaye Mungu, kwa kujua Kwake kabla, anajua wakati na ana mtumishi Wake hapo kuikemea dhambi.

105 Je! jiji hilo lenye ulimbwende lingeweza kumpokea? Unafikiri wanawake hao wangalijali yale aliyosema? Unafikiri makuhani hao wangalimsikiliza? Lo, la, bwana. Yeye hakuwa na barua yoyote ya sifa, kutoka kwa madhehebu yoyote. Asingeweza kusema, ya kwamba, "Mafarisayo walinituma." Wala asingeweza kusema ya kwamba Masadukayo walimtuma. Hakubeba vitambulisho vyovyote. Hakuwa na kadi yoyote ya ushirika kutoka kwa kundi lolote la watu. Hakuwa na mtangulizi wa kumwandalia kampeni yake. Hakukuwako na Mafarisayo wote waliofanya mkutano wa umoja na—na kiamshakinywa cha wahudumu, na wakatayarisha kila kitu, kuandaa kampeni yake, na wakijua ya kwamba alikuwa anakuja. Hakujulikana kwao. Hakuwa na kadi ya ushirika. Hakuwa na vitambulisho. Hakuwa na barua za sifa zake kutoka kwa wanadamu.

106 Bali alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Huo ndio mwenendo wa nabii wa kweli. Alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Kama alikuwa na BWANA ASEMA HIVI, ni kitu kilicho tofauti kabisa

na taratibu zetu za kujibunia hapa. Hilo tu ndilo alilohitaji. Kama akija jinsi *hii*, alikuja katika jina la kanisa fulani. Kama akitokea Huku, alikuja katika Jina la Bwana. Kwa hiyo, nabii wa kweli daima huja katika njia ya Jina la Bwana. Daima, anakuja katika Jina la Bwana.

107 Sasa, asingeweza kuonyesha kadi za ushirika, bali yeye—yeye alikuwa na Neno la Mungu. Na hilo ndilo ambalo Mungu alikuwa amewatumia watu. Sasa, watu walikuwa wamejiundia madhehebu. Walikuwa na makundi mbalimbali ya kimadhehebu, na hayo ndiyo watu walikuwa wameunda. Lakini Amosi hakuwa na kitu hicho. Yeye alikuwa tu na BWANA ASEMA HIVI. Hicho ndicho alichokuwa nacho.

108 Ningewazia hao makuhani, asubuhi moja, walikuwa na ninii ndogo asubuhi ya sabato, walikuwa na maombi madogo, kadhalika, ibada ndogo za kuweka wakfu, kisha—kisha wakarudi. Na wakazungumza mambo machache juu ya Musa mkuu, aliyeishi siku moja, na mtu mwingine mkuu aliyeishi siku moja. "Lakini, loo, siku za hao zimepita sasa. Ninyi watu mnamjua rais wetu mpya, serikali yetu mpya na yote tuliyo nayo," na kuzungumza juu ya mambo machache kama hayo kisha wakaenda nyumbani.

109 Lakini huyu hapa mtu anakuja asiyeyajali hayo. Alikuja na BWANA ASEMA HIVI. Unaona? Huo ndio mwenendo wa nabii. Hakuna ushirikiano, alijua kilichomkabili, alijua ya kwamba kila kitu kingempinga, alijua ya kwamba wangemkataa, wangemkatalia. Bali alikuwa akija katika Jina la Bwana.

110 Yesu alijua ya kwamba Kalvari ilikuwa ikimkabili, bali Yeye alikuja katika Jina la Bwana. Unaona? Huo ndio mwenendo wa nabii wa kweli.

111 Alikuwa na Neno la Bwana kwa ajili ya taifa hilo. Lakini Neno la kweli la Bwana lilikuwa ni geni kwa watu hao. Hata hivyo, walidhani walikuwa Nalo. Natumaini hili litazama ndani kwenye kilindi. Walidhani ya kwamba walikuwa watakatifu sana na wa kidini, hata Neno halisi la Mungu lilikuwa ni jambo geni kwao.

112 Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Neno la kweli la Mungu lililodhihirishwa ni jambo geni kwa Wapentekoste wengi. Fasiri halisi ya Neno, zile ole halisi, na laana, baraka halisi za Mungu ni jambo geni kwa watu wengi wanaojiita utakatifu, wafuasi wa kanisa, Wakristo. Ni jambo geni kwao. Hawalijui. Litaje kwao. "Sijapata kusikia jambo kama hilo." Na, hata hivyo, madhehebu yao yanakua na kufanikiwa, yanazidi kuwa na washiriki zaidi na zaidi wakati wote, na madhehebu zaidi yakiongezwa kila mwaka.

113 Walidhani ya kwamba kitu chochote kilichokuja kwao ilibidi kitokane na makundi hayo ya kimadhehebu. Hakika wasingempokea. Wala wasingempokea leo. Walikuwa

wamesahau kwa muda mrefu, ya kwamba, "Mungu alikuwa anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Mungu manabii wa kweli." Mungu anaweza, kwa watu wa huko nyuma mwituni. Anaweza kuinua, kutoka katika mawe haya, watu watakaolitetea Neno Lake, na kutabiri katika Jina Lake, ile Kweli. "Kuweka shoka kwenye shina la mti." Acha mambo yaive. Sijali kama ana ushirikiano ama hana ushirikiano. Lakini huo ndio mwenendo wa nabii wa kweli.

114 Watu wengine wanafikiri kazi yake ni rahisi. Hawajui wanalolizungumzia. Hakuletwa mjini kwa gari la farasi, akiketi juu ya farasi wazuri, wenye lijamu na hatamu, vishada, na makuhani wakuu wamesimama pale, wakiwa na vitu vikubwa na virefu vichwani mwao, wakimsujudia, "Mheshimiwa Dak. *Nanii* yuaja." Huo ungalikuwa ni mpangilio wa kimadhehebu.

115 Kama vile Mfalme wa hao wote alivyokuja, Yeye alikuja, kama, alipitia kwenye zizi katika kibanda, kibanda cha ng'ombe. Hakuja katika fahari na utukufu, bali alikuja katika unyenyekevu wa Mtoto Mchanga aliyezaliwa katika kibanda. Amosi hakuja . . . Neno la Bwana; maana yeye *alikuwa* Neno la Bwana. Neno lolote la Mungu, si mtu huyo; ni Mungu.

Yesu alisema, "Si Mimi ninayezitenda kazi hizi."

Walisema, "Wewe ni Mwanadamu, wajifanya Mwenyewe Mungu."

116 Akasema, "Basi kama sizifanyi kazi za Mungu, msiniamini Mimi. Lakini kama kazi zinajidhihirisha zenyewe, aminini hizo kazi, kama hamtaki kuniamini Mimi."

117 Amosi alikuwa ni Neno la Mungu lililokuwa likitembea barabarani. Aliingia, kishamba, si katika mtindo wa ulimwengu. Alikuja katika nguvu za Roho.

118 Hivyo ndivyo Neno la Mungu huja. Si katika kanuni ya imani ya kimadhehebu, si katika kitu fulani cha kidondoadume mimbarani; bali huja katika nguvu za Roho, kumdhihirisha Mungu kwa taifa na kwa watu. Ni tofauti. Ni tofauti jinsi gani!

119 Sasa, hawa walitambua, walisahau muda mrefu uliopita, ya kwamba Mungu anaweza kutoka kwenye mawe kuwainua manabii wa kweli. Haikuwapasa . . . Haikulibidi shirika lao kumwinua nabii wa kweli, maana labda lisingeweza kumwinua. Maana, kama lingalimwinua, angalikuwa ni nabii wa kimadhehebu.

120 Lakini, Mungu huinua! Mungu huchukua anachotaka. Yeye huchukua kilicho duni, kwa kawaida, kufanya kazi Yake; inaonyesha ya kwamba ni Mungu. Mtu anapojivuna sana, na kufikiri yeye ni kitu fulani, basi Mungu hawezi kumtumia, kwa sababu ana ubinafsi mwingi mno.

121 Hiyo ndiyo shida ya kanisa la Kikristo siku hizi. Wanafikiri wanajua jambo fulani. Biblia inasema, "Mtu anapofikiri anajua

jambo fulani, hajui lolote analopaswa kujua." Shida ya siku hizi, tuna ubinafsi mwingi mno, unafiki mwingi mno, elimu nyingi sana, dini nyingi sana, wala hatujui kitu juu ya wokovu wa Neno la Mungu. Hiyo ndiyo sehemu ya kuhuzunisha. Naam.

122 Walikuwa wamesahau, ya kwamba, "Mungu aliweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto, ama kuwainua manabii wa kweli wa Neno."

123 Haiwabidi kutoka katika shule fulani. Mungu huwafundisha. Haiwabidi kupata digrii nne chuoni. Haiwabidi kuwa na Shahada yao ya Kwanza, na—na Digrii yao ya Udaktari, na kadhalika. Haiwabidi kuwa na hiyo. Mungu huchukua chochote anachotaka Yeye, na kuweka Neno Lake ndani yake. Anafanyaje jambo hilo? Yeye hulidhihirisha na kulithibitisha.

124 Wasingeweza kusema Yesu alitokea kwenye seminari gani. Hakuwa na yoyote. "Anatokea shule gani?" Hakuwa na yoyote. Lakini Yeye alikuwa na kitu gani? Alikuwa na Mungu, na Yeye alikuwa ndiye Neno. Wasingeweza kurejea kwenye shule fulani.

125 Na Mungu hajapata kumwinua mtu kutoka shule fulani. Rudi kwenye historia uone ni mahali gani Yeye alipata kufanya hivyo. Hafanyi hivyo. Yeye huchukua kitu fulani kutoka mahali pengine, ambacho hakina kitu, hakina matumaini. Ndipo hukiingiza hicho ndani na kuliweka Neno Lake ndani yake, na kujidhihirisha Mwenyewe. Hivyo ndivyo alivyokuwa akifanya hapa katika Amosi. Vema.

126 Sasa, Neno la Amosi lilithibitishwa na Mungu, katika siku hiyo, katika siku zao wenyewe. Thibi-. . .Mungu alithibitisha Neno la Amosi kuwa, ya kwamba yeye alikuwa, alikuwa na Neno la Bwana.

127 Na kama angekuja kwetu, sasa hivi, je! mnafikiri taifa letu na watu wetu wangempokea mtu kama huyo? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Je! mnafikiri Wabaptisti wangempokea Amosi? ["La."] Wamethodisti? ["La."] Waprebiteri? ["La."] Wapentekoste? ["La."] Wakatoliki? ["La."] La, bwana. La. Bila shaka asingepokewa.

128 Hebu, kwa dakika moja, tumsafirishe na kumleta hapa, kwa dakika moja, tuone kama wangeweza ama wasingeweza. Hebu na tuone tu kama angeweza, kama makanisa yetu yangempokea leo ama hayangempokea.

129 Jambo la kwanza angefanya, angepinga kila dhehebu, maana liko kinyume na Neno. Naam, bwana. Angekataa mpango wetu wote. Hiyo ni kweli. Kila fundisho, kila kanuni ya imani, kila dhehebu, angekikataa kitu hicho chote.

Ninawazia tu, ninaweza kuona baadhi ya hawa wazee wa Kipentekoste wakisema, "Loo, utukufu kwa Mungu! Kama yeye. . .Loo, tusingemkaribisha mtu huyo mjini kwetu."

130 Na mnadhani Wapresbiteri na Wabaptisti wangefanya nini? "Mbona, mjinga huyo, hatumtaki nchini mwetu. Yeye si kitu ila mwe—mwenda wazimu." Wangetia sahihi karatasi kumweka gerezani, kama wangeweza, kumtoa mitaani.

131 Lakini unafikiri ungeweza kumshikilia pale? Loo, la. Huwezi kulifungia Neno la Mungu. La, la. Litajitokeza, kwa vyovyote vile. Milango ya gereza ilifunguka usiku mmoja, walipojaribu kulifungia. Nuru iliingia na kumtoa nje.

132 La, ye—yeye hakika angepinga mpango wetu. Vema. Angeanza kufanya nini? Kuubomoa. Kwa nini? Yeye ni mtumishi wa Mungu. Angeenda moja kwa moja kwenye Msingi na kuanza kampeni yake, moja kwa moja huko nyuma, na kurarua kila kanuni ya imani kutoka kwake, na kurudi kwenye Msingi wake. Msingi ni nini? Juu ya Neno la Mungu. Naam. "Mbingu na nchi zitapita, bali Maneno Yangu hayatapita." Kwa hiyo angerarua kila dhehebu, kila kanuni ya imani, kila fundisho, kutoka kwake, na kulitupa kando, na angelilipua liingie katika Umilele.

133 Unafikiri Wapentekoste wangempokea? La, bwana. Wabaptisti? Wapresbiteri? La, bwana. Wanazarayo? Wapilgrim Holiness? Wangemchukia. Hakika. Unafikiri wangetoka waende wakamlaki katika limuzini, na kumleta mjini? Wangeomba jua limuunguze kabisa huko juu. Wangeweka kizuizi, asiingie mjini. Mbona, kungekuwa na mikutano zaidi ya wahudumu kote, kote jijini, uliyopata kuona maishani mwako. "Msimruhusu mwenda wazimu huyo Kuingia jijini."

134 Lakini, hata hivyo, alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Unaona? Huo ndio mwenendo wa nabii wa kweli. Angedharauliwa. Hakika. Angerudi moja kwa moja kwenye Msingi, kwa ajili ya kampeni yake. Asingehitaji. Asingesema, "Sasa, ninataka ninyi Wamethodisti wote mwingie sasa na kunisaidia. Ninawatakeni ninyi Wabaptisti. Ninataka ninyi watu wote mlio karibu hapa. Ninyi Wapentekoste wote, mnadai ya kwamba ninyi ndio kikundi cha mwisho ambacho Mungu atakiita, ninawatakeni ninyi nyote mje kwangu, na ninataka muunge mkono kampeni yangu."

135 "Mnabatizaje? Ushahidi wa kwanza wa Roho Mtakatifu ni upi?" Maswali hayo, yangetupwa usoni mwake. Na akirudi na Ukweli wa Biblia, wangemkataa. Lakini huo ndio mwenendo wa nabii wa kweli. Ana hayo yote ya kukabiliana nayo. Unaona? Hakika.

136 Tusingempokea. La, bwana. Ninii yetu—yetu... Tusingekuwa na yoyote. Hatutaruhusu kampeni zake zozote kote katika nchi ye—yetu. La, hasha. Vema, tusingemtaka. La, bwana. Lakini angekuja na kulirudisha Kanisa kwenye Neno, kwa kuwa Huo ndio msingi. "Yeyote atakayeweka msingi mwingine wowote, ni mchanga unaodidimia. Juu ya msingi *huu*

peke yake, Mungu analijenga Kanisa Lake, juu ya Fundisho la mitume."

137 Kama nilivyokuwa nikisema hivi majuzi; mtu fulani akizungumza kuhusu—kuhusu toharani, na kurejea kwa wengi kama vile Mtakatifu Francis na Mtakatifu Cecilia, naye akiwaombea watu fulani, na kuwatoa toharani, na kuwapa mamlaka kama hayo. Hayo ni mamlaka yasiyo ya kimaandiko. Ni watu wasio na mamlaka. Mitume walikuwa na mamlaka ya Kimaandiko. Na kama ni kinyume nao, ni uongo, nijuavyo mimi.

138 Kweli ninaamini katika toharani, bali ninaamini ni sasa hivi. Unaisafisha nafsi yako mwenyewe. *Toharani* maana yake ni "kusafisha kabisa." Unapoona umefanya kosa, toka huko nje na ulisafishe likutoke, kwa kukiri, na kulia, na kufunga, na kuomba.

139 Mtu fulani hata alinicheka wakati Bwana alipokuja hapa si muda mrefu uliopita na kunipa ono. Daima nilitaka kuona jinsi ya kumfunga yule nyoka. Daima nilijiuliza jinsi ya kumfunga. Ninapaswa kupiga hatua namna hiyo. Wakati, hilo ndilo nimetaka, maishani mwangu mwote. Ndipo nikaanza kufunga na kuomba. Kasema, "Unafanya hivyo kwa nini?"

140 Nikasema, "Katika jambo hilo, Yeye alisema sikuwa mwaminifu vya kutosha." Baada ya Yeye kuja, ndipo nilitaka kujitakasa mwenyewe. Si kungoja mpaka utakapokufa, na kuacha kasisi fulani ajaribu kukutakasa. Takaseni nafsi zenu!

141 Lakini, unaona, walilichukua kutoka kwenye Neno lenye mamlaka, na kuliweka mikononi mwa mafundisho ya sharti ya kujibunia, wapate kuleta pesa kanisani, kwa sababu wanaangalia mambo ya kilimwengu, kanisa la kilimwengu, nguvu kuu ulimwenguni, nguvu za kisiasa. Lakini Mungu huliangalia Neno Lake. Na neno lolote ambalo ni kinyume cha Neno la Mungu ni makosa. Nionavyo mimi, ni Neno ama si lolote. Naam, bwana. Naam, bwana.

142 Yeye angeenda moja kwa moja kwenye ule Msingi. Angekirarua kitu hicho vipande-vipande. Ingemlazimu kufanya hivyo. Asingeweza kufanya jambo lingine lolote, kama Amosi angalikuwa hapa leo. Asingeweza kufanya jambo lingine lolote, kwa maana, kumbukeni, yeye ni nabii wa kweli wa Mungu, ambaye hujiliwa na Neno. Asingeweza kufanya jambo lingine lolote ila kurudi kwenye Neno. Haidhuru kama Wapentekoste wote nchini walikusanyika kumzunguka, waseme, "Bwana, Amosi, tunakuamini wewe kuwa ni nabii, bali uko nje ya Neno. Tunataka kukunyosha." Yeye angedumu na Neno. Hakuna kitu kingine angaliweza kufanya, kwa sababu yeye ni nabii. Hakuhitaji ushirikiano wao. Yeye ana Ujumbe wa kutoa. "Na wote alionipa Baba watanijia Mimi." Naye anaenda kuhubiri

Neno, naye atalihubiri jinsi tu lingekuwa katika Biblia, na kwa hivyo tungemkataa. Hiyo ni kweli.

143 Haidhuru ingekuwa nini, Neno la Mungu huwajia manabii, fasiri yao ya Neno, fasiri halisi.

144 Israeli daima walitoka kwenye mstari, na Mungu aliwatumia nabii pamoja na ishara na maajabu, kulifasiri hilo Neno. Naye alijuaje? Yeye alisema, "Kama nabii huyu akinena, na linatimia, basi hilo ni kweli." Yeye aliwathibitisha manabii Wake, ya kwamba walikuwa sahihi.

145 Yesu alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya. Kwa njia hii mtajua. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

146 Nao wanawezaje kudai kuwa ni nabii wa Bwana na kukana Neno lenyewe la Mungu? Mtu anawezaje kubatiza katika jina la "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," hivyo vyeo, na kukana Jina lenyewe la Yesu Kristo, wakati hakuna Maandiko katika Biblia yanayounga mkono nadharia yao? Huenda nikawa mkali na mkosoaji, bali wakati wa kuwa hivyo umewadia. Ni Kweli.

147 Watu wanawezaje kudai kwamba ni Wakristo leo, na kukimbilia kila kitu hapa nje; na wanawake wakiwa na nywele zilizokatwa, na kuvaa kaptura, na kuvuta sigara, na kukimbilia kwenye sinema, na namna yoyote ya maonyesho ya kale, na kufanya yasiyofaa? Mwaniambia huyo ni Roho Mtakatifu? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Kamwe msiniambie hivyo. Ninyi, mnamfanya Mungu achefuke tumboni Mwake, kama jambo kama hilo lingeweza kutendeka. Naam. Nina hakika mnafahamu. Mnajiita, kitu kama hicho, kunawezaje kuwepo na kitu kama hicho? "Kwa matunda yao wanatambulikana."

148 Yeye angelikemea na kulaani kila mwanamke aliyekata nywele zake. Angewezaje kufanya jambo lingine lolote? Yeye ni nabii. Na hilo ni Neno. Angesema, "Enyi, Mayezebeli!" Angewakemea. Kwa nini? Yeye ni nabii. Ingembidi kudumu na Neno. Hiyo ni kweli. Unafikiri wangeacha? La, bwana. Wangesema, "Ni ulokole. Yeye ni mbaya kama maskini yule Paulo wa kale alivyokuwa, katika Biblia, mchukia-wanawake."

149 "Ninyi, kundi la waigaji, mnaojiita Wakristo. Haidhuru mnajaribu kuishi watakatifu jinsi gani, hilo halina uhusiano wowote nalo. Mradi tu unakana Neno la Mungu wala hujiweki sawa Nalo, wewe ni mwenye dhambi, asiyeamini," hivyo ndivyo yeye angesema. Asingeninii . . . Kuweka, angeweka shoka moja kwa moja kwenye shina la mti. Asingeachilia chochote. Yeye ni nabii, na huo ndio mwenendo wa nabii wa kweli. Wangedumu kwa hilo Neno haidhuru ni nani. Kama ni mama yao wenyewe ama baba; haileti tofauti yoyote. Yesu alifanya hivyo. Hata asingemwita yeye mama; yeye hakuwa mama. Yeye alikuwa Mungu. Mungu hana mama. Wangekuwa, basi baba Yake ni nani? A-ha, a-ha.

150 Yeye angewalipua na kuwakaripia. Angekaripia kila dhehebu, kwa sababu hakuna hata moja la hayo lililojengwa juu ya Neno. Siwezi kupata hata moja la hayo. Na mara wanapofanya madhehebu, wako kinyume na Neno papo hapo. Kwa hiyo inawezekanaje. . . nabii kubariki kile ambacho Neno linalaani? Hata hivyo, yeye hataki kufanya hivyo, kumuudhi ndugu yake, lakini hata hivyo inampasa kufanya hivyo kwa sababu yeye ni nabii. Naye ni wakilisho la Neno la kweli la Mungu, wala haondoki Kwalo, hata kidogo; amri juu ya amri, na kanuni juu ya kanuni. Unaona ninalomaanisha? Mwenendo wa nabii wa kweli.

151 Ni wangapi wanasema, "Bwana, laiti ungalinifanya mimi nabii"? Yeye hafanyi hivyo. La. Hafanyi hivyo.

152 Angekaripia kila tendo baya la makanisa, karamu hizi za kudanganyana na mambo haya yote waliyo nayo, karamu za kadi, mlo wa supu. Angekemea kila moja ya hizo. Angezilipua ziingie kuzimu zinakotoka.

153 Mnafikiri mngempokea? La. Kanisa leo lisingempokea. Pentekoste impokee? Vema, angeingia mle ndani, aseme, "Enyi kundi la Mayezebeli mliokata nywele, hivi hamjui maana ya BWANA ASEMA HIVI? Mnatembea nje hapa mkiwa na maskini nguo fupi iliyobana sana, hivi hamjui mna hatia ya kufanya uzinzi kila siku na mamia ya wanaume." Hivyo ndivyo angesema.

154 Mnasema, "Vema, maskini mzee mbumbumbu! Maskini mzee upara, mwenye mvi, mwondoeni kwenye hiyo mimbara. Hebu tuwaone ninyi, halmashauri ya wadhamini, mashemasi, mkimwondosha hapa."

155 "Vema, enyi kundi la wanafiki wenye mashaka." Kweli. Amosi angepiga kelele. Halafu mnajiita, "Sisi ni. . . Sisi ni wafuasi wa kundi *hili*. Sisi ni wafuasi wa kundi *lile*." Ninyi ni wa ibilisi, baba yenu, kwa kuwa yeye ndiye anayekana Neno.

156 Unasema, "Nilinena kwa lugha." Halafu ukate nywele zako? "Utukufu kwa Mungu! Haleluya!" Nayo Biblia ilisema, "Ni ninii—ni jambo la—la kawaida, kwa mwanamke kuomba akiwa amenyoa kichwa chake namna hiyo." Kisha unajiita Mkristo. Ona aibu. Jikokote pembeni mahali fulani, ujiweke sawa na Mungu.

157 Unavaa maskini nguo hizo ndogo fupi, kisha unatoka unaenda hapa nje uwanjani, na kujianika, huku ukijua vizuri sana unafanya uzinzi na wanaume mia moja kila siku. Kasema, Yesu alisema hivyo, "Mtu amwangaliaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kufanya uzinzi naye." Mwanamke ndiye aliyejianika, nawe ukafanya hivyo katika ninii yako. . .

158 Ambapo, wewe, umekufa kwa mambo ya ulimwengu. Umefufuliwa kutoka kwenye hayo, kama nilivyosema, mwanzoni. "Ungegeuza kichwa chako katika aibu. Macho

yako yanafinyaa juu ya kitu kibaya kama hicho cha dhambi, badala ya kuwaangalia wanawake kuwatamani. Ninyi wanaume mnaofanya jambo kama hilo na kujiita Wakristo." Hivyo ndivyo angewaambia. Ninajaribu kuchukua maneno yake asubuhi ya leo. Yangekuwa ni Maneno yake. Kwa kuwa, yeye, kumbukeni, yeye ni nabii wa kweli. Ingembidi kudumu na Neno hilo. A-ha. Ninayanukuu tu Maneno yake. Hivyo tu. Maana, kama mlimleta, yeye ni Neno. Halafu, hili hapa Neno, Lenyewe. Huenda msiwe na mtu huyo, bali mna Neno Lake, kwa kuwa angekuwa na Neno la Bwana.

159 Kila fundisho la kujibunia, angelililaani, kama vile ubatizo "katika jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Angetupilia kitu hicho moja kwa moja kukirejesha katika umilele. Angekilaumu, kwa hiyo kusingekuwako na harufu yake iliyosalia. Naam, bwana.

160 Ni wangapi, ninyi, ni wangapi kanisani humu asubuhi ya leo wangempokea kwa jambo hilo?

161 Ndipo wao, kundi hili la Jina la Yesu, wange—wangesema, "Loo, tungemshambulia juu ya hilo." Halafu dhehebu lenu, angewalipua moja kwa moja pamoja nalo. Hiyo ni kweli. Wanawake wenu waliokata nywele, nanyi mnavumilia jambo hilo. Hiyo ni kweli. Wanaume wenu, jinsi wanavyofanya na kutenda. Hiyo ni kweli.

162 Watu wengi husema, "Ni vizuri kuwa nabii." Ni sawa, kama uko tayari kuuza kila kitu kwa ulimwengu na udumu na Mungu na Neno Lake.

163 La, hatungempokea kwa vyovyote vile, madhehebu yetu leo. Hakika tusingekuwa na uhusiano wowote naye.

164 Msikilizeni akilipua hayo. Alisema, "Mungu yeye yule mnayedai mnamwamini, Yeye atawaangamiza." Mtafanya nini juu ya jambo hilo? Mungu yeye yule Pentekoste inayemwamini, kutokana na yale matendo yenyewe ya utovu wa uadilifu na mambo wanayofanya na kuyaruhusu yafanywe, Mungu yuyo huyo ataleta hukumu juu ya hayo madhehebu. Hiyo ni kweli. Ndivyo hasa Amosi alivyowaambia.

165 "Loo," wao walisema, "tuna Ibrahimu. Tuna—tuna *hili*. Tuna torati. Tuna makuhani. Tuna manabii."

166 Loo, ndugu, hayo macho yalifinyaa wakati akiwaangalia, na kuwakaripia kwa hilo Neno. Naam, bwana. Hakika. Wasingempokea. La, bwana. Yeye alisema, "Watawaangamiza kwa mafundisho yenu ya kujibunia." Hivyo ndivyo angewaambia leo. Angesema vile vile alivyosema wakati huo. Yeye alisema, "Mungu yeye yule mnayemjengea makanisa, labda mnalipia mamilioni ya dola, madhabahu zizo hizo mnazomjengea Yehova, ambaye mnadai kwamba mnampenda, Mungu yuyo huyo atawaangamiza kwa sababu mnalikataa Neno Lake."

167 Vivyo hivyo na leo hii! Mungu yeye yule ambaye Marekani inadai kumtumikia ataleta hukumu juu ya taifa hili na kuliangamiza. Ninatumaini hilo linakolea sana hata hamtaweza kufurukuta mtoke kwake. Yeye yule mnayedai ya kwamba mnampenda, na pamoja na mafundisho yenu ya sharti ya kujibunia, na maisha machafu na uozo mlio nao, mkiwa mbali na Neno la Mungu, atawaangamiza siku moja. Hilo ni BWANA ASEMA HIVI. Hakuna kitu kingine kinachowabakia.

168 Jiwekeni sawa na Neno! Unawahubiria Injili; unaenda kote nchini; unawaambia Ukweli. Wahudumu wanazozana na kupiga makelele, na kufanya yasiyofaa. Wanaume wanakuhukumu. Madhehebu yanakufukuza. Wanawake wanatikisa kichwa chao, wala wasingeacha nywele zao zikue, kwa chochote kile. Wanavaa nguo vile vile tu kabisa, mwaka baada ya mwaka. Ni kama tu kumimina maji juu ya mgongo wa bata. "Kisha mnadai mnampenda Mungu?"

169 Yeye alisema, Yesu alisema, "Mmechukua mapokeo yenu na kuzitangua Amri za Mungu."

170 Huo ndio mwenendo wa nabii wa kweli. Unaona? Si njia rahisi. Si vile kila mtu anavyofikiri ingeweza kuwa.

171 Wanarukaruka na kupiga mayowe, kila mtu akikupigapiga begani kukupongeza, basi hiyo ni ishara ya kwamba wewe si nabii wa kweli. Hiyo ni moja ya ishara halisi ya kwamba huna kile unachonena habari zake.

172 Ni lini walipompigapiga mgongoni kumpongeza, isipokuwa wawe walikuwa na sababu zao? Ati nini? Yeye angegeuka na kuwakaripia. Kweli. Wasingempigapiga Amosi mgongoni kumsifu. Wasingempigapiga Eliya mgongoni kumsifu. Yeye hakuuvumilia upuuzi huo. La, bwana. Aliwaambia Ukweli wa Mungu. Na kama Mbingu ni kuu sana, na mahali tunakoelekea, basi kama hatuwezi kujiweka sawa na mambo madogo-madogo sana, tutajiwekaje sawa na Roho Pale? Inatupasa kujiweka sawa na Neno. Huo ndio mwenendo wa nabii wa kweli. Ingawa lilimrarua vipande-vipande, kulisema, naam, hana budi kulirarua taifa vipande-vipande, kwa Hilo. Hiyo ni kweli. Lakini hiyo ndiyo njia.

173 Yeye angekemea jambo hilo. Loo, jamani! Unajua alilowaambia? "Misukosuko," kama ukiangalia hapa, yeye alisema, "haiko katika serikali yenu, iko ndani yenu." Hayo ndiyo aliyosema. Naam. "Misukosuko kanisani, mfano wenu wa utauwa, hayo ndiyo yaliyovuruga mambo."

174 Sababu ya ukomunisti kuenea nchini leo, si kwa sababu ya ukomunisti. Ni kwa sababu ya kanisa. Ni kwa sababu ya watu. Leo wanajiita Mkristo. Wanaimba kama Malaika. Sauti zilizofanyiwa mazoezi, na wanazungumza kwa ufasaha sana, kana kwamba wao walikuwa ni Malaika Wakuu; nao hawaliamini Neno la Mungu, kama mashetani. Hiyo ni kweli.

Wanaimba kama Malaika Mkuu, wanavaa kama sijui-ni-kitu-gani, na kulikana Neno la Mungu.

175 Mwanamume, mhubiri mimbarani, ambaye atasimama pale na kuitwa Daktari, Kasisi, na umuulize, "Je! Biblia ilinena juu ya ubatizo katika 'Jina la Bwana Yesu Kristo,' ama 'Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu'?" Naye atacheka mbele yako na kuchukua "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Halafu ati ujiite mtoto wa Mungu?

176 Wanawake wakijua ya kwamba Biblia inawakataza kufanya mambo fulani, na kukata nywele zao, na kuenenda kama ulimwengu, na kuvaa nguo chafu na vitu kama hivyo, nao watafanya hivyo daima, kwa vyovyote vile; na kunena kwa lugha, na kurukaruka, na kupaza sauti, na kuwa na umoja wa mama wazee, na mashirika ya kushona, na kuwatuma wamishenari hudumani. Imekuwa harufu mbaya sana mbele za Mungu. Na, BWANA ASEMA HIVI, Yeye atakiangamiza kitu hicho chote. Atakiangamiza.

177 Si jambo rahisi, bali huo ndio mwenendo wa nabii wa kweli. Atakilipulia mbali huko nje, na kulinena kama linaudhi ama haliudhi.

178 Yohana alikuwa nabii wa kweli. Alisema, "Shoka limewekwa kwenye shina la mti." Huo ndio mwenendo wao. Hakika.

179 Shida iko ndani ya hilo. Wanaimba kama Malaika, wanacheza kama pepo hapa nje, madansi, wanafanya yasiyofaa, kucheza karata, mbio za farasi. Wapentekoste, wakienda mahali pa burudani, sinema zimejaa wao. Kila mahali, namna yoyote ya mchezo wa kale ama chochote kile, na wanashuka moja kwa moja wanaenda kule chini, na mashindano ya mbio na chochote kile, na kujiita Wakristo, na kwenda huko na kupiga makelele, na kunena kwa lugha, na kushiriki katika kutawadha miguu na ushirika.

180 Mbona, ni—ni, "Kama mbwa anavyoyaendea matapiko yake," nabii alisema, "nao ni vivyo hivyo." Kama kitu hicho kilikuwa ni cha ulimwengu, ilibidi kitupwe kitoke ndani yako, kwa nini unakirudia tena? Kweli. Huko nje mitaani, wakinenguanengua, wanavyoiita, roki, wakikata nywele, wakivaa kaptura. Loo, jamani! Wanajiita Wakristo. Ungeweza . . . La, afadhali nisiseme hilo.

181 Hiyo ndiyo sababu ninawakemea. Kama nitadumu na Neno *hili*, kama Neno hili likinijia, nitadumu na Neno hili. Hili ndilo linalonijia mimi, Neno. Kukemea jambo hilo!

182 Anadai kuongozwa na Roho Mtakatifu, na anafanya mambo kama hayo. Ungeweza kuwazia mwanamke, akiongozwa na Roho Mtakatifu, kuachilia nywele zake zikatwe, wakati Roho Mtakatifu mwenyewe analikataa jambo hilo? Basi Roho Mtakatifu ni Mtu wa aina gani? Ungeweza kuwazia?

183 Ungeweza kuwazia mhubiri akisimama mimbarani, na mtu yeyote ampe changamoto kumwonyesha mahali pamoja mtu yeyote aliwahi kubatizwa akitumia vyeo vya “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” na kukucheka waziwazi na kukuita mlokole, kwa kubatiza katika Jina la Yesu Kristo, na kusema anaongozwa na Roho, na kusema ya kwamba ana Roho Mtakatifu? Je! Roho Mtakatifu angeweza kukana Neno Lake Mwenyewe? La, bwana. A-ha. Mnaona? Natumaini mnalipata.

184 Sijui ni muda gani. Mlipuko unaofuata huenda ukanipata. Lakini, mpaka utakaponipata, nitakuwa nikisimama pale pale na Neno. Nitakapokutana nanyi huko ng’ambo kwenye ile Hukumu, nitakuwa nimesimama moja kwa moja karibu na hilo Neno. Hilo ndilo ninaloamini kwamba ni Kweli.

185 La, hufanyi mambo kama hayo, halafu uwe na Roho Mtakatifu. Nilienda kwa mke wa mhudumu fulani wakati mmoja, ameketi pale akiwa amevaa rinda, lilikuwa likionekana ni la kihuni.

Unasema, “Huna haki zozote.”

186 Nina haki. Hilo ni Neno. Lihubiri lote. Mnayakwepa mambo hayo, wahubiri wengi madondoadume, kwa maana hawana ujasi- . . . Labda hata hujaitwa kuhubiri, kwanza. Naam. Lakini mtumishi halisi wa Mungu atadumu moja kwa moja na Neno hilo. Kweli.

187 Mke wa mhudumu akiketi pale, amebanwa sana na rinda, na vipuli vikining’inia, na amejipodoa, na nywele fupi zilizokatwa. Wakati, Mungu anakikataa kitu hicho chote kama uchafu. Na halafu unasema ati una Roho Mtakatifu?

188 Nilikuwa nikihubiri hapa Phoenix, si muda mrefu uliopita, juu ya jambo kama hilo, na mke wa mhudumu akiketi mimbarani, akiwa na mtindo huo wa kivulana wa kukata nywele pindokombo, na akiwa na nguo ambayo asingeweza kuzuia sketi zake za ndani kuonekana wazi. Asingeweza kuivuta juu ya magoti yake. Kama inchi nne ama tano juu ya magoti yake, ameketi pale; akirukaruka, akiongoza nyimbo. Nilikemea jambo hilo sana jinsi nilivyoweza. Bila shaka, hatanialika nirudi tena. Sitarajii kualikwa. Lakini yeye anajua yaliyo kweli na yaliyo uongo. Nitakaposimama Hukumuni, haliko mkononi mwangu tena. Kisha wanaondoka na kusema . . .

189 Mtu, anayedaiwa ni mwalimu, ambaye sisemi lakini yeye siye, alitoa tamshi hivi majuzi, mbele ya baadhi ya marafiki zangu kwenye jiji fulani nilimokuwa. Mnamjua ndugu huyo. Basi huyu ndugu akaingia. Akasema, vema, akasema, “Tulikuwa na Ndugu Branham hapa wakati mmoja.” Jiji fulani, na ni huko Magharibi. Naye mtu huyu akasema, “Loo, Ndugu Branham ni mtu mzuri.” Unaona? Alijua vema kuliko kutupa chochote juu ya sifa. Kasema, “Ndugu Branham, bali msisikilize kanda zake, kwa sababu zitawachanganya.”

190 Na ilitokea kulikuwa na mmoja wa marafiki zangu alikuwa amesimama pale, kasema, "Hebu kidogo, bwana! Nilikuwa nimechanganyikiwa mpaka *nilipozisikiliza* hizo kanda." Naam. Hiyo ndiyo tofauti. "Nisingeweza kufahamu jinsi ambavyo Mungu mtakatifu angevumilia mambo kama hayo, kama yale mnayofanya ninyi nyote." Naam.

191 Mtu yule yule, mwingine aliyekuwa pamoja naye, alisimama mahali fulani si muda mrefu uliopita, kasema, "Ndugu Branham ni nabii. Anaweza kuyatambua mambo. Na vitu kama . . . Lakini," kasema, "sasa, msisisikilize Fundisho lake, maana yeye si sahihi." Wazimu huo, matamshi ya kishenzi namna hiyo!

192 Hivi hamjui ya kwamba kama ni nanii . . . Mimi si nabii. Lakini kama Neno la Mungu ni kweli, linamjia nabii. "Neno la Bwana liliwajia manabii." Hao ndio waliolifasiri Neno. Halafu, unaona, huninii . . .

193 Hata haileti maana, kujificha tu nyuma ya madhehebu fulani madogomadogo, moja ya siku hizo yatavunjika na kuliwa na kutu, na kuangamia katika kuzimu.

194 Lakini Neno la Mungu litadumu milele. Juu ya Mwamba huo ninajenga matumaini yangu milele, juu ya Neno la Bwana. Acha kila kitu kingine chochote kizame. Kama nikimpoteza kila rafiki, vyovyote vingine, urafiki wangu ni katika Kristo.

> Matumaini yangu hayajajengwa juu ya kitu chochote pungufu
> Ila Maneno ya Kristo na haki Yake;
> Wakati yote yanayonizunguka yanapoporomoka,
> Ndipo Yeye Ndiye tumaini langu lote pamoja na mahali pa kutia nanga.

195 Hiyo bunduki ililipuka hivi majuzi. Niliiona. Nilidhani nilikuwa nimekufa. Nilijisikia nimejaa amani. Niliangalia kote. Nikawazia, "Vema, yamenifika." Dhehebu lingenifaidia nini wakati huo? Shirika lingenifaidia nini wakati huo? Ingenibidi kusimama huko ng'ambo kwenye hukumu za Mungu zinazowaka moto, kuhukumiwa kwa Neno *hili*.

196 Ingawa ilinibidi kuwaunguza, na kuwapinda, na kuwanyonganyonga, na kuwararua, watu wengi, lakini ninatumaini kufanya, kupata kiini halisi kutoka humo, cha Neno la Mungu, na hapo niijenge nafsi kwa ajili ya Umilele. Hiyo ni kweli. Hebu Mungu aiweke mikononi Mwake na kuijenga kuwa mtoto mtiifu.

197 Mtu angewezaje—mtu angewezaje, anayeongozwa na Roho Mtakatifu, kufanya jambo kama hilo? Ama, mwanamke aliye na Roho Mtakatifu, kufanya mambo kama hayo? La. Yeye ni mtakatifu. Na kama Uzima Wake umo ndani yako, wewe uko vivyo hivyo. Utakuwa kama Yeye tu.

198 Israeli, kama sisi, walifikiri kwa sababu walikuwa wakifanikiwa kwa ushirikiano na wengine eti, kwamba hilo lilikuwa ndicho kibali cha Mungu kwa jambo hilo. Sasa, mnajua, tunafikiri hivyo leo.

199 Nilizungumza na wanaume fulani hapa si muda mrefu uliopita, kwenye hoteli, siku chache zilizopita, watu wakubwa katika milki ya kidini. Nao wakaniambia, "Mungu anathibitisha ya kwamba Yeye yuko pamoja nasi. Mbona, tuliongezeka mwaka uliopita, Ndugu Branham," nasahau ni mamia mangapi, namna hiyo.

200 Nikasema, "Hilo si thibitisho hata kidogo." A-ha. Hiyo ni kweli. Ukahaba umestawi, uliongezeka mwaka jana, kama asilimia thelathini; je! hilo lilionyesha Mungu alikuwa pamoja na ukahaba? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] A-ha. A-ha. A-ha. Hakika. En-he! Hoja hiyo haifai kitu. La. Huwezi kufanya hivyo. La, bwana. Mungu husimama na Neno Lake. Mtu mwingine yeyote atasimama na Neno Lake, kama yeye ni mwaminifu. Vema.

201 Walidhani, kwa sababu walikuwa na ushirikiano! Sasa, hapa, tutaingia, kwa muda kidogo tu, katika mambo ya serikali. Taifa letu limelikataa Neno la Mungu, kama tu vile Israeli walivyofanya. Walilikataa Neno la Mungu, na watu wao, makuhani wao, na manabii, na kadhalika, wanatabiri mazuri kwao. Na wao. . .Tunaweza kufanya nini ila kutabiri mabaya, kwa maana ni kinyume cha Neno! Limeangamia. "Taifa letu kuu, tunalolipenda, lililowekwa msingi juu ya ninii. . .ujuzi wetu wa babu zetu." Basi rejeeni kwa yale waliyokuwa nayo. A-ha. Kweli. Hakika.

202 Israeli walikuwa ni taifa kuu. Waangalie babu zao, lakini Mungu hakuwahurumia. Huyo nabii mzee kipara alikuwa akiwatupia Neno, na lilitimia vile vile juu ya alama kama alivyosema. Someni historia yenu hapa mpate kujua kama si kweli. Lilikuja kutimia vile vile kabisa jinsi alivyosema. Na aliwahukumu, hata hivyo, wao wakisimama pale, na makuhani watakatifu waliovaa mavazi matakatifu, wakinyunyizia *hiki*; wala wasingesogeza mkono, upande *huu* wala upande *ule*, kwa maana lilikuwa ni jambo fulani namna *hii*, mila ama kitu fulani.

203 Yesu alisema, "Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi, na kazi zake mtazifanya." Walimchukua na kumhukumu, na kumtundika juu ya mti, na kumwua. Kweli kabisa. Mungu alimfufua tena. Naam, bwana.

204 La, wasingeweza. Tusingemwamini Amosi leo, hata kidogo. Na leo tumefanya muungano. Tuna kile tunachoita leo. . . Tunafikiri ni "kibali" cha Mungu, kwa sababu madhehebu yetu yanapanuka na—na kila kitu kinaenda jinsi kinavyoenda. Tunafikiri hicho ni "kibali" cha Mungu kwa jambo hilo. Unajua, waliungana, ninaamini, Waprotestanti kama milioni mbili ama

tatu zaidi. Na Wakatoliki wameongezeka mamilioni kadhaa zaidi. Unaona? Wanafikiri hicho ni kibali cha Mungu, kwa wao kuwa Wakatoliki. Waprotestanti wanafikiri hicho ni kibali cha Mungu, wao wakiwa Waprotestanti. A-ha! Ni upuuzi. Ni chakula cha mizinga. Ni majivu ya atomiki. Ni hasira ya Mungu inayofura, ipate kulipuka. Hiyo ni kweli kabisa.

Nisikilizeni. Nitawaambia Neno la Bwana. Amina.

205 Hebu na tujiangalie. Angalieni ulimwengu siku hizi. Angalieni taifa letu. Tumeungana na U.M. Una nini ndani yake? Kundi la wasiomcha Mungu. Na sisi, huku tukiwa na ujasiri wa kutoruhusu hata kuomba kabla ya kuanza kikao chetu.

206 Hivi mimi hivi punde sikusoma hapa, "Watu wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipopatana? Mungu hatendi neno pasipo kuwafunulia watumishi Wake, manabii. Watu wawili wanawezaje kutembea wasipopatana."

207 Wakati, tuna Waislamu, Wabudha, makafiri, wasiomcha Mungu, wachoyo, chochote kile, ndani yake. Mnafikiri—mnafikiri Mungu angeweza kuishi katika kitu kama hicho?

208 "Vema," mnasema, "hilo, vema, tuna mapatano nao. Tuna ulinzi wote wa Magharibi."

209 Walikuwa na mataifa yote jirani, wakiwalinda. Lakini nabii huyo alisema, "Mungu atawaangamiza. Mungu yeye yule mnayemtumikia atawaangamiza, kwa ajili ya ujinga wenu." Angesema jambo lile lile asubuhi ya leo. Angewakemea sana, kutoka Ikulu hadi kufikia kwenye shamba la maskini. Hakika angewakemea. Angewakemea, kwa Neno la Mungu. Hakika angewakemea. Huo ndio mwenendo wa nabii wa kweli.

210 "Hebu na tujitazame tulivyo, makanisa. Loo, sisi ni kanisa kuu takatifu la Katoliki la Kirumi!" Limenenwa, katika Biblia, kuwa ni KAHABA.

211 "Sisi ni wale wazee wa baba zetu, makanisa ya Kiprotestanti, sote tumeungana pamoja, na kuitwa ninii . . . linaitwa Baraza la Makanisa Ulimwenguni." Makahaba wa huyo KAHABA mkuu, Biblia ilisema. Hivyo ndivyo hasa ilivyosema. A-ha. Na hata hivyo tunafikiri, "Na sasa makanisa yote yanaungana pamoja."

212 Bw. Collins, rafiki yangu, ndugu kutoka California, Arizona pale. Ninii—ninii yako . . . [Ndugu Neville anasema, "Elmer."—Mh.] Elmer. Nilisema, "Vema, nadhani unahudhuria kanisa fulani zuri dogo la Kimethodisti."

213 Kasema, "Nililiacha wakati walipojiunga na Baraza la Makanisa kule juu."

214 Nikasema, "Mungu akubariki. Unaukaribia ule Ufalme, ndugu." A-ha. Naam, bwana.

215 Fundisho la sharti, wakitegemea ushirikiano wa wanadamu, pamoja na fundisho lao la kujibunia, na kuliacha Neno la Mungu. Tunachohitaji ni nabii leo, alilipulie hilo Neno mle ndani. Ndivyo hasa. Naam.

216 Wao, wanachukua usalama miongoni mwao. "Loo, tulijiunga. Sisi, Wapentekoste, hakika, tulijiunga na Baraza la Makanisa Ulimwenguni, kwa sababu mle ndani tuna ushirika. Tutawavuta waje." Ni kama mwanamke anayekwenda kwenye chumba cha pombe, akalewe pamoja na mumewe, apate kumvuta kwa Mungu. Zaidi sana ni kama mume akienda pamoja na mke wake, siku hizi, kwenye baa, wakalewe, apate kumvuta kwa Mungu. Upuuzi! Kaa mbali na eneo la ibilisi.

217 Wakati kitu chochote kinapolikana Neno hilo, mimi ninakipinga. Hilo linanifanya kuyapinga madhehebu yote, maana yanalipinga Neno. Linapaswa kumfanya kila mwaminio kujisikia hivyo. A-ha!

"Vema," wanasema, "lakini, kumbukeni, tuna ninii . . . "

218 Nina dondooo kubwa kutoka kwenye gazeti, mtu fulani alinitumia kutoka Arizona, juu ya jinsi ambavyo huyu mzee *Nanii*, hivi majuzi, alivyosema, "Papa Yohana wa Ishirini na Mbili," ama vyovyote wanavyomwita, "alikuwa . . . Yeye ni mtu mzuri. Yeye ndiye mtu pekee aliyewahi kuzungumza juu ya kuyaunganisha makanisa, Wakatoliki na Waprotestanti, pamoja." Kasema, "Huenda hilo lisitukie katika siku zetu, bali, miaka kumi na mitano ama ishirini ijayo, jambo hili litatimia."

219 Nikawaza, "Jamani, wewe ukiwa ni mzee, unatabiri, wala hujui hilo."

220 "Wakati umeenda kuliko tunavyowazia." Yule jamaa aliyeniandikia, aliandika juu ya ukurasa huo, "Wakati umeenda kuliko tunavyowazia." Alikuwa akisikiliza kanda, pia. Naam, bwana. Yeye alisema, "Wakati umeenda kuliko tunavyowazia." Kasema, "Ndugu Branham, si ulisema jambo hili, miaka kadhaa iliyopita?"

221 Nikasema, "Hakika." Naam, bwana. Linaenda kutimia, kwa sababu ni Neno la Bwana. Halina budi kutimia. Hakika. Naam.

222 Wanasema, "Vema, huyu mzee mtakatifu, hivi hudhani anapaswa kujua jambo fulani zaidi ya hilo?" La, bwana. Kama anakana Neno la Mungu, analiangalia namna hiyo, hawezi.

223 Sijali ni mapapa wangapi, manabii, na kitu gani zaidi mlicho nacho miongoni mwenu. Kama mko nje ya Neno, ninyi mko nje ya Neno. Hiyo ni kweli. Mungu angewezaje kubariki kitu kama hicho, mradi tu wanakana Neno lenyewe la Mungu? Yeye anawezaje kubariki chochote mbali na Neno Lake, kitu ambacho ni kinyume na Neno Lake? Anawezaje kulikana?

224 Unawezaje kubariki kansa inayokutafuna? Ungewezaje kubariki waya wa—wa—wa umeme ambao umeushika, unasema, "Loo, nishike na unichome"? Huo ungekuwa ni wazimu.

225 Mungu anawezaje kubariki chochote ambacho ni kinyume na Neno Lake? Kwa hiyo rudi kwenye Neno! A-ha.

226 Enyi kundi la wahubiri, kama mbwa wakubwa wa kuwinda, mna shida gani? Mnatoka mnaenda hapa nje na kuuza haki zenu za mzaliwa wa kwanza kwa chakula cha mchuzi wa nyama na mboga, mpate kuendesha Kadilaki ama kitu kama hicho, ama jumba kubwa mno mahali fulani, na kanisa kubwa la dola milioni moja. Na mambo hayo yote namna hiyo, na kuuza haki zenu za mzaliwa wa kwanza, na mnaona aibu na mnaogopa kulihubiri Neno la Mungu kwa kusanyiko lenu. Aisee, hivi hamjionei aibu? Na kujiita mwenyewe mtumishi, nabii wa Mungu, huku mkiuza haki zenu za mzaliwa wa kwanza kwa riziki ya mambo ya ulimwengu. Mtaangua kitu gani? Kama kile Esau alichoangua. Loo, ni aibu jinsi gani!

227 Loo, la! Mungu mtakatifu ambaye hulinda Neno Lake, kulithibitisha, asingeweza kubariki kitu ambacho ni kinyume na Neno Lake. Sasa sikilizeni. Ninajua ninachelewa kidogo tu, na huenda ninawakaba roho mpaka mkaribie kufa. Lakini, angalieni, ninataka kuwauliza jambo fulani. Mungu mtakatifu angewezaje, aliyenena Neno Lake na kusema, "Sasa, mbingu na nchi zitapita, bali Hilo halitapita, si hata Neno moja Lake," sasa anawezaje kuchukua kitu ambacho ni kinyume cha Hilo na kukibariki? Angewezaje kufanya jambo hilo? Angalia. Yeye anathibitisha, Yeye Mwenyewe. Yeye huthibitisha Neno Lake. Anasema yaliyo kweli, sio kwa uanachama.

228 Angalia Moabu. Moabu alikuwa na Neno Lake, pia, Moabu. Israeli walikuwa na Neno Lake; na Moabu walikuwa na mfano wa utauwa, na Neno Lake. Walitoa dhabihu saba, fahali safi, juu ya madhabahu saba; nambari kamilifu, dhabihu kamilifu. Halafu, mbali na hayo, aliwachukua kondoo dume saba, zikinena ya kwamba waliamini katika kuja kwa Mwana wa Mungu, na kuwatoa sadaka pale, pamoja na askofu wao mkuu. Watu wao wote mashuhuri, makuhani wao wote na makuhani wakuu, chochote kile, walisimama pale pamoja na wafalme wao na marais, na wowote wale, na kuitoa hii kwa kidini tu walivyoweza, dhidi ya Israeli.

229 Nao Israeli walikuwa kule chini, kundi dogo la mahaini, jinsi walivyoonekana. Lakini Israeli walikuwa na kitu gani? Mungu alikuwa katika uamsho wao. Alikuwa akijithibitisha, kwamba alikuwa pamoja nao. Unaona?

230 Haidhuru wangekuwa na wazee wangapi, mapapa, ama chochote kile, Mungu hawezi kuwa pamoja nao mpaka ajithibitishe kwamba Yuko pamoja nao. Na mradi tu wako nje ya Neno Lake, na kulikana Neno Lake, Yeye anawezaje

kuwa pamoja nao? Hakuna ishara za Mungu aliye hai miongoni mwao.

231 Mungu angewezaje kuwa miongoni mwa U.M., wakati wawili hawawezi kutembea pamoja wasipopatana?

232 Sasa, angalieni hapa. Kuna kanisa la Kristo, linavyojiita, lililoungana na Wapentekoste. Wapentekoste wanasema wanaamini katika kunena kwa lugha. Wanaamini katika thibitisho la Roho Mtakatifu, kunena kwa lugha. Wanasema wanaamini katika *hili*, *lile*, na *linginelo*. Wanaamini katika ishara na maajabu. Kanisa la Kristo linawacheka, wakasema, "Enyi kundi la wajinga! Hayo yalikuwa ni ya siku zilizopita." Watu wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipopatana? Nao waliungana pamoja. Wanafanya nini? Wanatafuta usalama wa wao kwa wao. Tupilieni mbali upuuzi kama huo!

233 Usalama wangu uko katika Kristo na katika Neno Lake, kwa maana Neno Lake ni Yeye Mwenyewe. Hiyo ni kweli.

Hakuna ishara za Mungu aliye hai, hata kidogo.

234 Hivyo ndivyo Yesu alivyosema, "Kama silidhihirishi Neno, basi msiliamini. Kama Mungu haneni na kutoa unabii kupitia Kwangu, na kusema kupitia Kwangu na kutenda kupitia Kwangu yale hasa Masihi anayopaswa kufanya, basi msiniamini."

235 Halafu, jamaa fulani anasema ya kwamba yeye ni nabii aliyetumwa kutoka kwa Mungu, na kulikana Neno? Mungu na arehemu kwa upuuzi kama huo! Mungu anawezaje kufanya jambo kama hilo?

236 Hebu niulize, niulize, jambo hili sasa. Si—sijui ni wakati gani nitakapozungumza na ninyi tena. Hilo lingekuwa ni juu ya Mungu. Ninaweka tu Chakula, kama vile alivyoniambia katika lile ono wakati ule, kukiweka katika mapipa.

237 Huenda mkaniuliza mimi, "Amosi angewezaje kuona kabla kile kitakachowapata?" Mbona, lilionekana ni salama.

238 Angalieni. Sasa angalieni hapa. Sasa, sikilizeni kwa makini sasa. Maana, Haya yote yako kwenye kanda, na yataenda, yataenda kote ulimwenguni. Mnaona? Sasa vipi . . . Angalieni hapa.

239 Hao hapo Israeli. Seminari zao zilikuwa katika hali bora zaidi kuliko zilivyopata kuwa. Hakuna mtu anayewasumbua. Walikuwa na dini zao wenyewe. Hakuna mtu yeyote aliyesema, "Hamwezi kumwabudu Yehova." "Endeleeni," yakasema mataifa hayo makafiri, "mkaabudu. Tuna mapatano, mmoja kwa mwingine."

240 Nabii huyo aling'amua hayo. Unaona? Vivyo hivyo na nabii wa sasa atang'amua hayo. Unaona?

241 "Endeleeni." Nao Israeli wakasema, "Vema, hebu na tule, tunywe, na tufurahi." Kwa hiyo wakakusanya kundi pamoja na kujifanyia kanuni za imani, na mashirika, madhehebu, na kadhalika, na kujiweka vizuri vilivyo. Nao wanawake wao waliishi tu kwa anasa na dhambi huko nje. Jamani, wakibebwa kote kwenye mikahawa wakawatumbuize watu na kila kitu, nusu uchi, wamevaa sketi ndogo za hariri inayoona. Kama ulipata kuona baadhi ya ninii yao—historia yao ya siku hizo, jinsi walivyoonekana, loo, karibu theluthi moja ya ubaya walio nao leo. Sio kabisa, hata hivyo, kwa maana wasingeweza kuwa hivyo. Naam. Na jinsi walivyofanya na kufanya yasiyofaa namna hiyo; na wafalme, na makuhani, na yeyote yule.

242 Yesu alisema, "Mnakula nyumba za wajane, enyi wanafiki." Alisema hivyo. Na mambo haya yote waliyokuwa wakifanya.

243 Huyo nabii akisimama pale, akiangalia hilo, hilo taifa namna hiyo, si ajabu moyo wake uliraruliwa toka kwake. Naam, bwana.

244 Sasa, mnasema, "Alijuaje kile kilichokuwa kinaenda kutukia? Yeye angewezaje kutangulia kukiona hapo awali? Vipi?" Yote yalionekana ni mazuri. Kwa nini, walikuwa na chakula tele. Walikuwa na nguo tele. Wao, walikuwa na makanisa yao makubwa. Wanafanikiwa. Fedha zimepandwa kila mahali, anasa. Madansi mitaani, uzinzi, na kila kitu kikiendelea tu, na kila kitu kinaendelea vizuri. Kama tu Marekani leo. Televisheni imejaa mizaha michafu, wanawake nusu uchi, chochote kile. Kila kitu unachoona ni uchafu tu na dhambi. Haikubidi kuangalia televisheni, fungua tu macho yako, angalia popote pale. Wasichana, wavulana, wanaume, wanawake; kuvuta sigara, kunywa pombe. Hao Mayezebeli wakijiita wenyewe Wakristo. Pepo wachafu wakijiita wenyewe Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Katoliki, na Wapentekoste. A-ha. A-ha.

Si ajabu macho yake yalifinyaa wakati alipoangalia. A-ha! Hiyo ni kweli.

245 "Yote yanaonekana ni mazuri. Unawezaje kuokoa kitu hicho? Kama tutaenda kufanya . . . Vipi? Vipi? Angalia hapa. Vema, sisi—sisi tuna milioni moja zaidi. Sisi—sisi tuna . . . Sisi . . . Majengo yetu ni, loo, makanisa yetu ni makubwa sana, inatubidi kujenga makanisa mapya. Vema, tuna fedha nyingi sana, hatujui la kufanya nazo. Mbona, tunajenga tu mahali palipo pazuri sana katika—katika taifa. Makanisa makubwa sana yaliyopo, ni yetu. Na tungali tuna fedha nyingi sana. Hivi hamwoni Mungu ametubariki?" La. Mko nje ya Neno Lake.

246 "Na, Ndugu Branham, unamaanisha Mungu ataliangamiza hili?" Naam, kila moja yao.

"Unajuaje?" Amosi, ulijuaje?

247 Ni kama tu daktari akibaini ugonjwa. Wakati anapoupata ugonjwa alio nao mgonjwa, anajua la kufanya. Anajua

huyo mgonjwa ana nini. Anajua umeenea kiasi gani. Na anajua litakalotukia. Hivyo ndivyo ilivyo kwa nabii, nabii wa kweli, wakati anapoona. Sijali unalofanya. Wakati anapoona dhambi ikienea, ni kansa inayokula. Na imeenea sana, katika Wapentekoste na hao wengine wote, haiwezi kurudi. Imefikia hatua mbaya sana. Wataangamia.

248 Hivyo ndivyo jinsi Amosi angeweza kubaini hali hiyo. Aliitambua kwa Neno la Mungu. Hivyo ndivyo na—nabii wa kweli huitambua hali, na kuwaambia hao wanawake, "Kamwe msijaribu kwenda hukumuni na nywele zilizokatwa, wakati mkijua vyema linalofaa." Anawaambia ninyi wanaume, ninyi wengine, na ninyi wahubiri mnaolikana Neno, na wenye mfano wa utauwa, na kujiunga na madhehebu, kukwepa suala hilo, wakati mkijua vema linalofaa. Mnaangalia Neno lile lile manabii wa kweli wangeliangalia. Utambuzi wa jambo hilo ulisema, "Mauti! Utengano!" Ni kama tu daktari, yeye anajua ugonjwa huo. Anajua dalili ulizo nazo.

249 Angalia taifa hili. Wakati unaposema, "Pentekoste imekwisha." Wakati, hata hawatakuacha uje kanisani, sababu unawahubiria wanawake kuhusu nywele zilizokatwa, na Biblia inalaani jambo hilo. Wanahofu utasema jambo fulani kuhusu . . .

250 Hapa hivi majuzi, wakati nilipokuwa nikiandaa miamsho kadhaa, Roy Borders alipokuwa akiziandaa, kwenye Pwani ya Magharibi, walimkusanyia, kundi la wahudumu, wakiwa karibu, loo, nakisia arobaini ama hamsini, ambako nilikuwa na mkutano mkubwa. Wakasema, "Bw. Borders, ninataka kukuuliza jambo fulani." Wakasema, "Je! ni kweli kwamba Ndugu Branham anatumia Jina la Bwana Yesu Kristo kubatizia?"

251 Bw. Borders, mwungwana mheshimiwa sana, kama mumjuavyo Ndugu Borders kutoka hapa. Akasema, "Mabwana," akasema, "Ndugu Branham, wakati akiwa huko nje kwenye kampeni, huko nje, hii," kasema, "yeye hahubiri. Yeye anaenda tu moja kwa moja na kuwaombea wagonjwa wenu. Hivyo ndivyo kadiri anavyofanya."

252 Kasema, "Hivyo sivyo nilivyokuuliza," kasema mzee wa kanisa. "Yeye hubatiza hivyo?" Sasa, walikuwa na zile kanda. Wanajua. Kasema, "Je! yeye hubatiza katika Jina la Yesu Kristo?"

253 Akasema, "Ndiyo, katika kanisa lake mwenyewe. Hapo ndipo mahali pekee anapobatizia, katika kanisa lake mwenyewe.

254 Akasema, "Haya basi. Hivyo tu ndivyo ninavyotaka kujua. Hatumtaki. Hatutaki uzushi huo miongoni mwa watu wetu."

255 Na hivi majuzi, wakati rafiki yangu msiri, Ed Daulton, alipopata barua kutoka kwenye kanisa la Kibaptisti. Yeye alisema, "Tunakufukuza kutoka katika ushirika wa Kibaptisti,

kwa kuwa umejiunga kwenye uzushi wa kubatizwa katika Jina la Yesu."

256 Ninapenda kusimama pamoja na Paulo, "Katika kile ulimwengu unachoita uzushi, hivyo ndivyo ninavyomwabudu Mungu, maana ni Neno Lake." Naam, bwana. Naam. Loo, hakika.

257 Daktari hubaini ugonjwa. Anaona mahali ulipo. Nabii wa kweli hubaini hali, kwa Neno. Anafanya nini? Daktari hutambua ugonjwa wa mtu, kwa dalili. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yeye huangalia dalili na kuona shida ya mgonjwa ni nini. Anaona umeenea kiasi gani, na kusema, "Hakuna kinachoweza kufanywa."

258 Naye nabii wa kweli hulichukua Neno la Mungu na kuyabaini magonjwa, anayatupia Dawa. Nao watu wanamrushia usoni mwake. Ni jambo gani litakalotukia? Kuangamia, hivyo tu; kundi la wapenda anasa, wenye dalili ya kilimwengu wanaoitwa unafiki! Lakini huo ndio mwenendo wa nabii wa kweli. Mnaona? Loo, jamani!

259 Yeye anaona magonjwa. Aliona ya kwamba waliliacha Neno. Yeye aliliona Neno. Na alijua matokeo yaliyokuwa yanakuja. Aliona anasa waliyokuwa wakiishi ndani yake, aliona jinsi hao wanawake walivyokuwa wakitenda. Aliona jinsi hao makuhani walivyokuwa wakifanya, jinsi walivyoiacha ibada ya kweli ya Mungu, na mambo kama hayo. Hapo, alipata ninii—alipata jibu. Alisema, "Huyo Mungu mnayedai mtamtumikia atawaangamiza."

"Kwa nini?"

260 "Hamkuzishika Amri Zangu." Na hata hivyo walidhani alikuwa amezishika. Hivi mimi sikusoma jambo hilo hapa? Kifungu cha 2, cha 4 . . . Mlango wa 2, kifungu cha 4, "Kwa sababu niliwachagua kuwa ninii . . . Kati ya jamii zote za dunia, niliwachagua, na hata hivyo mnakataa kutembea katika Amri Zangu." Mnafikiri . . .

261 Maskini, nabii huyu mdogo mwenye upara aliyesimama pale na ndevu zenye mvi zikifanya milia machoni mwake, zikimulika kama moto, akizungumza na kundi hilo la makuhani na kadhalika, na kusema, "Mungu ambaye ninyi wanafiki mnafanya kana kwamba mnamtumikia, Mungu yuyo huyo atawaangamiza." Unafikiri angepata ushirikiano? A-ha! Akasema . . . Loo, jamani! Yeye, mjaribu leo uone kama angepata ushirikiano. La. Lakini vipi yeye? Huo ndio mwenendo wa nabii wa kweli. Alikuwa na Neno. Alijua lilikuwa ni kitu gani.

Kama vile Mikaya wa kale . . .

262 Mtoto yule mchanga niliyemweka wakfu, niliruka mengine, dakika chache zilizopita, maana niliharakisha wakati.

263 Lakini, Mikaya, wakati aliposimama mbele za Ahabu, aliwaangalia. Alijua Neno. Mikaya aliwaambia Neno. Kwa nini? Mikaya alichunguza ono lake, Fundisho lake, kwa Neno la Mungu. Naye akaona ya kwamba Fundisho lake na Neno vilikuwa vinakubaliana. Kwa sababu, Neno lilisema Yeye angemlaani Ahabu, na angewafanya mbwa kuilamba damu yake. Hivyo ndivyo Neno lilivyosema.

264 Kwa hiyo, Mikaya alikuwa na ono. Hiyo ni kusema, alikuwa ni nabii. "Mnaona ni Neno gani hunijia." Naye akaomba, "Ee Bwana Mungu, nifanyeje? Niliambie nini kundi hili la wahubiri linalosimama hapa? Haya hapa madhehebu yote. Kila mtu nchini amekusanyika dhidi yangu, Bwana. Mimi hapa nimesimama mbele ya mfalme. Niseme nini?"

265 Ndipo akaingia katika ono. Kasema, "Kweeni. Endeleeni." Kasema, "Bali niliona Israeli wametawanyika kama kondoo wasio na mchungaji." Naam.

266 Huyo—huyo mzee wa wilaya alimwendea na kumpiga kofi mdomoni, na kusema, "Neno la Mungu, Roho wa Mungu, alienda wapi, alipotoka kwangu?" Kutoka kwake?

267 Unajua kile Mungu alichosema? Alimwacha pepo ashuke aende, aingie miongoni mwao, kwa maana walikuwa nje ya Neno, kwanza.

268 Biblia ilisema, "Wasipoliamini Neno, Yeye atawaletea nguvu za upotevu, kuamini uongo, na wahukumiwe kwa huo." Hivyo ndivyo hasa madhehebu haya na watu wa taifa hili wanavyofanya leo, wanaamini uongo, wapate kuhukumiwa kwa huo. "Kwa kuwa hapana Jina jingine chini ya Mbingu walilopewa litupasalo kuokolewa kwalo." Jiwekeni sawa, enyi madhehebu, na kadhalika. Naam.

269 Sasa, ni kitu gani hawa wengine walininii. . .?. . .Manabii hawa wengine waliangalia nini? Walikuwa manabii. Naam, bwana. Walikuwa manabii. Lakini laiti wangalitulia na kuchunguza unabii wao kwa Neno!

270 Laiti Wamethodisti wangetulia leo na kuchunguza unabii wao, wasingemnyunyizia mtu mwingine. Wangempokea Roho Mtakatifu. Wangembatiza kila mtu kwa kumzamisha, katika Jina la Yesu Kristo. Laiti Assemblies of God wangetulia leo na kuchunguza unabii wao, wangerudi kwenye Neno. Laiti wa Umoja, leo, wangetulia na kuchunguza unabii wao, wangerudi kwenye Neno.

271 Lakini, unaona, laiti hao manabii wangalitulia na kuchunguza unabii wao! Walihoji. Walisema, "Hiyo ni yetu. Kwa hiyo tutakwea kwenda Ramothi-Giliadi na tutaiteka, kwa sababu ni yetu. Yoshua alitupa hiyo."

Lakini Mikaya akasema, "Hilo linaonekana kwamba ni la busara."

272 Lakini hivyo ndivyo ilivyo. Hutaki kutoa hoja. Unataka kuamini yale Mungu aliyosema. Usitoe hoja yoyote.

273 Vipi kama Ibrahimu angalihoji? Angaliwezaje kuondoka nchini mwake? Angewezaje kuwa na umri wa miaka mia moja, angali akimsifu Mungu, nao wakienda kumpata mtoto kwa Sara, naye akiwa na miaka tisini?

Tupilia mbali hoja. Amini tu.

274 Unamwacha ibilisi akwambie, "Unajua, Ndugu Branham si kitu ila mnafiki."

275 "Sasa, sasa nangojea, hebu nione kama ndivyo alivyo. Hebu tuone kama anafundisha vizuri. Hebu nirudi kwenye Biblia." Usininii, usiende. . . Hatakuruhusu kufanya hivyo. La, la. Unaona?

276 Lakini atasema jambo fulani baya kunihusu mimi, ambalo huenda akawa na haki ya kusema, ndipo unaendelea tu kupata hilo, kusimama na kuanza kuhoji, "Naam. Hakupaswa kufanya jambo *hili*. Hakupaswa kufanya *lile*." Ukianza kuniangalia, vema, utakuwa na mengi sana.

277 Pia ungepata ukimwangalia Bwana Yesu. Unaweza kupata mengi. Mwangalie, kidogo. Nitamfanya kila mmoja wenu mhudumu. Sasa tutasahau Yeye aliwahi kuwa duniani. Huyu hapa Mvulana ambaye amethibitishwa, kote nchini, ya kwamba Yeye ni Mtoto wa kuzaliwa ha—haramu. Mama yake alimpata kabla yeye na baba Yake hawajafunga ndoa. Imethibitishwa. (Sasa, hawaendi kwenye Neno, "Bikira atachukua mimba.") Wanaenda tu na yale wanayosikia, unaona, "Mwana haramu." Hivi wao hawakumwambia, "Alizaliwa katika dhambi, na ati anajaribu kuwafundisha"? Mimi ni . . . Unaona?

278 Pia angalia yale aliyokuwa akifanya. Alikuwa kweli akirarua kila kanisa lililokuwako nchini. Hiyo ilikuwa ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Madhehebu, chochote kile.

279 Yeye alikuwa ni nani? "Mvulana tu aliyekua upesi mno akienda kote namna hiyo, Jamaa mdogo, hana dhehebu. Niambie wewe ni mfuasi wa kanisa gani. Baba Yako ni nani? Ati unasema Yusufu si baba Yako?"

"Yusufu si baba Yangu," Yeye angesema.

"Vema, Baba Yako ni nani?"

"Mungu ndiye Baba Yangu."

280 "Vema, Ewe mlokole! Hivyo ndivyo ulivyo hasa. Wewe, ukiwa Mwanadamu, na kusema Mungu ndiye Baba Yako?"

281 Laiti wangalikuwa wamelichunguza kwa Neno! Haleluya. Hivi hamwoni ni nini? Neno lilikuwa lifanyike mwili. Hawakuchunguza ono lao kwa Neno. Jambo ndilo hilo.

282 Hiyo ndiyo shida ya siku hizi. Hamchunguzi maono yenu kwa ninii. . .unabii we—wenu na fundisho lenu, kwa Neno la Mungu. Mtu akijaribu kuwaambia Kweli, basi mnakosana nao, kama tu vile Amosi angalifanya, Amosi alivyofanya. Mnafanya jambo lile lile.

283 Sasa angalieni hapa. Yeye yuko katika hali hii. Sasa, mngalimhukumu, labda, hiyo ni kweli, kama hamkuwa mmerudi kwenye Neno. Wanafanya vivyo hivyo. Wanamhukumu siku hizi.

284 Vipi kama ninyi wanawake, *hapa* na *hapa*, naam, mbona hamwangalii wazo lenu la kukata nywele kwa Neno, na mwone vile linavyosema? Mnaona? Kwa nini hamfanyi mambo hayo?

285 Kwa nini msichunguze ubatizo wenu, wa "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," huo "utatu" wa uongo, unavyoitwa, ambao si kitu ulimwenguni ila ofisi tatu za Mungu mmoja, vyeo? Sio *jina* la "Baba." Hakuna kitu kama *jina*, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu."

286 Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, ambalo ni, "Bwana Yesu Kristo." Chunguza ubatizo wako na jinsi kila mtu katika Biblia anavyobatizwa. Kama ungechunguza wazo lako kwa Neno, u—ungerudi na kubatizwa katika Jina la "Bwana Yesu Kristo."

287 Hivyo ndivyo Paulo alivyowaambia wafanye. Na akasema, "Kama mtu mwingine yeyote akifundisha jambo lolote tofauti, na—na alaaniwe, hata kama Malaika akishuka chini."

288 Mnajua, mara nyingi, Malaika wanashuka. Jamani, jinsi Wapentekoste wanavyomeza hilo!

289 Vipi kuhusu wakati Mtakatifu Martin alipokuwa amesimama pale, na hapa kilisimama kiumbe kikubwa cheupe mbele yake?

290 Mtu aliyebatiza katika Jina la Yesu, ambaye aliamini katika Roho Mtakatifu, na alidumu na Neno! Na Warumi wakimfukuza, na wakimfanyia kila kitu, wakijaribu kumpa mafundisho yao ya sharti na mafundisho ya kujibunia. Mtu huyo alisimama kwenye Neno.

291 Siku moja, katika nguvu zake, pepo wangemjia na kujaribu kuzungumza naye. Asingewasikiliza hata kidogo.

292 Siku moja, Shetani alikuja namna hiyo, kama Kristo, amevikwa taji, amevaa sapatu za dhahabu, akasimama pale na kusema, "Usininii. . ." Miali ya moto imemzunguka. Kasema, "Hivi hunitambui Mimi, Martin? Mimi ni Bwana wako. Niabudu Mimi."

Martin akamwangalia. "Kuna kasoro fulani pale."

293 Akasema, "Martin, hivi huwezi kunitambua?" Kasema, "Mimi ni Bwana na Mwokozi Wako." Kasema, "Niabudu." Akasema hivyo mara tatu.

294 Ndipo Martin akaangalia kila mahali. Akaona, Kristo atavikwa taji na watu Wake, hapo atakapokuja. Hatakuwa amevaa sapatu za dhahabu. Akasema, "Ondoka mbele zangu, Shetani."

Jamani, Wapentekoste si wangemeza hilo? "Jamani, Malaika anayeng'aa na kuwaka!"

295 Yule mwanamke alishuka akaja, Chicago mahali ninapoenda, kasema, "Ndugu Branham, wahudumu huko juu walisema kama Malaika wa Bwana alikwambia ubatize katika Jina la Yesu, wangeukubali. Lakini je! hilo ni wazo lako mwenyewe?"

296 Nikasema, "Malaika wa Bwana akisema lolote kinyume cha Hilo, asingekuwa ni Malaika wa Bwana." Unaona?

297 Kama Malaika yeyote akisema lolote ambalo ni kinyume na Neno *hili*, na liwe ni uongo. Na kama mtu akiwaambia, mjumbe kutoka kwa Mungu, akisema ametoka kwa Mungu, na kuwaambia, "Ni sawa kubatizwa, jina la 'Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,'" na awe mwongo.

298 Kama mtu akikwambia, "Ni sawa kwako, uwe na nywele zilizokatwa, na mambo kama hayo; ya kwamba unapaswa kuvaa kofia kanisani, boneti, 'kiwe ndicho kifuniko,'" na awe mwongo.

299 Neno la Mungu, ndilo Kweli. Yoyote ya mambo haya ambayo yanapinga Neno, na yawe uongo. Ni Neno, ndilo Kweli. Litasimama.

300 Hiyo ndiyo sababu Mikaya angeweza kujua ya kwamba unabii wake ulitoka kwa Mungu, kwa sababu ulikuwa unakubaliana na Neno la Mungu. Naam, bwana. Ono lake liliafikiana kabisa na Neno la Mungu.

301 Loo, kama Amosi angalikuwa hapa, yeye angedumu na Neno. Hiyo ni kweli. Lakini, unaona, shida ya siku hizi, kwetu sisi, ni kama ilivyo kwao. Niko karibu kufunga. Shida yetu ni kama waliyokuwa nayo. Walikuwa wamefundishwa, nje ya ule Msingi. Yesu alisema, "Mmelitangua Neno la Mungu kwa mapokeo yenu." Na huo ubatizo wa uongo! Hiyo ishara ya uongo ya kumpokea Roho Mtakatifu! Baadhi yao walisema, "Peaneni mkono." Baadhi yao walisema, "Nena kwa lugha." Nimeyasikia mashetani yakinena kwa lugha, na kupeana mikono, pia. Naam, bwana. Sio ishara Yake. Sasa, mambo haya yote namna hiyo, mambo hayo yote, unaona, mnaliacha Neno la Mungu kufundisha mapokeo hayo. Hiyo ni kweli.

Sasa, yeye angeninii, ingembidi kuwarudisha kwenye Neno.

302 Lakini tunaninii, waalimu wetu siku hizi, wamewafundisha watu, nje ya ule Msingi wa Neno la Mungu. Sasa sikilizeni kwa makini.

303 Hivyo ndivyo walivyokuwa wamefanya kule. Hivyo ndivyo Amosi alivyokuwa akiwaambia. "Mungu mnayedai kumjua, Yeye Ndiye atakayewaangamiza."

304 Sasa, tumewafundisha, nje ya (kitu gani?) Msingi wa "Imani waliyokabidhiwa baba wa kipentekoste mara moja," naam, Biblia. Tulifundisha toharani ya uongo! Tulifundisha ubatizo wa uongo! Kila kitu, uongo, uongo, uongo, tukijitenga na yale ya Asili.

305 Ati hamwamini jambo hilo? Rudini kwenye Biblia, na mchukue "toharani" yenu, na mchukue "Baba, Mwana, Roho Matakatifu" wenu, na "kunyunyizia," na upuuzi huo wote, na mrudi mwone kama ni la Kimaandiko. Hiyo ndiyo njia. Tafuteni kujua kama liko juu ya ule Msingi. Unaona? Wako nje ya ule Msingi.

306 Ambapo, Paulo alisema jambo hilo, Biblia. Biblia inazungumza juu ya jambo hilo, ni—ninii. . .ya kwamba, "Kanisa la Mungu limejengwa juu ya Fundisho la mitume na manabii." Manabii na mitume hawana budi kuwa kitu kimoja. Hakika.

307 Ati nini? Tulitoka kwenye ule Msingi wa Neno, tukaingia kwenye misingi ya kimadhehebu.

308 Sikilizeni sasa. Ninafunga. Vaeni kisaidizi cha usikivu wenu wa kiroho. Sikilizeni.

309 Tumeondoka kwenye Msingi wa Neno, tukaenda kwenye msingi wa dhehebu fulani. Ningeweza kukaa kwenye jambo hilo kwa muda gani? Saa zingine tatu. Kutoka nje ya Msingi wa Neno, kuingia kwenye msingi wa anasa za dunia, ulimwengu, utovu wa uadilifu ukinyemelea kuingia kanisani. Kutoka kwenye Neno, kuingia kwenye kanuni za imani. Hilo lingenichukua majuma matatu kulihubiri lote, kufikia nusu yake, hayo matamshi manne papo hapo. Kutoka kwenye Neno, kuingia kwenye dhehebu, neno la kidhehebu. Mara—mara tu kanisa linapounda dhehebu, liko nje ya Neno papo hapo.

310 Hakuna ila jambo moja. Kurudi moja kwa moja mahali lilipoliachia, na liende tena. Lirudi kwenye Neno. Hiyo ni kweli. *Kutubu* maana yake ni "kwenda, kurudi nyuma, kugeuka." Unaelekea njia mbaya. Vema.

311 Dhehebu la anasa. Dhehebu la kuabu-. . .M—msingi, ninamaanisha, wa—wa anasa, msingi wa mambo ya ulimwengu, msingi wa kanuni za imani. Na yote hayo, pamoja, yaliangua upotovu wa maadili, upotovu wa kiroho.

312 Yeye akiwa ni nabii wa kweli, angeona kwetu yale yale aliyoona kwao. Kama alikuwa amesimama hapa juu ya jukwaa hili leo, nami ningesema, "Ndugu Amosi, nabii mkuu wa Mungu, wewe usiyeogopa, njoo hapa uchukue mahali pangu," yeye angehubiri Neno hili. Ingembidi kufanya hivyo. Yeye ni

nabii. Vema. Angelilihubiri jinsi tu lilivyoandikwa, vile vile tu tunavyosema sasa. Vema. Angekuwa akiona basi kile alichoona ndani yetu, utovu wa uadilifu.

313 Angalieni tu, marafiki. Ni wangapi hapa, katika kanisa hili lililo hapa sasa, wanaoona ya kwamba ulimwengu uko katika uozo wa uadilifu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mbona, tunajua uko hivyo. Kuna shida gani? Uko nje ya Neno. Kweli. Vema.

314 Amosi kamwe hakuilaumu serikali. Je! mlimwona hapa, mtakapolisoma mtakapoenda nyumbani? Yeye hakuilaumu serikali, alililaumu kanisa kwa kuichagua serikali kama hiyo. A-ha!

315 Ninyi wanasiasa, hebu niache hilo lisagwe ndani yenu kwa muda kidogo, hapa na kote ulimwenguni, mahali litakapoenda. Kanisa lilimchagua mtu kama Yeroboamu. Sijui kama ninyi, sisi, hivi hatujafanya karibu jambo lile lile? Hebu na tuseme ni serikali nzuri; serikali haiwezi kujenga nyumba juu ya mwamba wakati watu wanachagua nyumba juu ya mchanga. Sivyo? Msiseme, "Serikali yetu! Serikali yetu!" Ni ninyi, taifa. Ni watu. Tunawezaje . . .

316 Mhudumu aliniambia, kasema, "Ndugu Branham," kasema, "angalia. Ninajua wewe uko sahihi katika jambo Hilo. Lakini," kasema, "kama ningehubiri Hilo, dhehebu langu lingenitupa nje, watu wangu wangenifukuza kanisani." Kasema, "Sitahubiri mahubiri mengine kamwe."

Nikasema, "Lihubiri, kwa vyovyote vile." Naam, bwana.

317 Ni Neno la Mungu. Wewe unawajibika. Kama wewe ni nabii wa Mungu, wa kweli, utadumu na Neno. Kama sivyo, utadumu na dhehebu lako. Inategemea umetoka wapi.

318 Angalia. La, bwana. Hatuwezi kujenga, serikali haiwezi kujenga nyumba juu ya Mwamba imara wakati watu wanapigia kura nyumba ya anasa juu ya mchanga udidimiao.

319 Angalia kile tunachotaka. Hebu tuchukue dakika moja sasa. Natumaini siwachoshi. [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Lakini hebu na tuangalie kile tunachotaka, kwa dakika moja. Siwezi kuacha tamshi hili, muhtasari huu. Angalia kile tunachotaka.

320 Angalia televisheni yetu. Hilo ndilo tunalotaka. Tunataka baadhi ya hawa wachekeshaji kusimama pale na kuleta kila namna ya mizaha michafu, nasi tunakaa nyumbani kuacha kwenda kwenye mikutano ya maombi Jumatano usiku, ama mhubiri anawaruhusu mtoke mapema ili kwamba mweze kwenda mkaangalie; kahaba fulani, mbembe, mchafu, aliyeolewa mara tano ama sita, akitoa mizaha michafu, amevalia kizinifu, na akiendelea kufanya vitendo vibaya kama nini. Nanyi mnapenda jambo hilo zaidi kuliko mnavyoipenda nyumba ya Mungu, inaonyesha ni aina gani ya roho iliyo ndani yenu.

321 Tunaruhusu. Sisi, watu, kama watu wa taifa hili wangeandika barua kwa serikali yetu, tuseme kungekuwa na barua milioni mia moja zilizorushiwa kwenda kwenye serikali hiyo, "Komesheni vipindi hivyo vichafu," ingewalazimu kufanya hivyo. Sisi ndio watu. Lakini sisi, watu, tunataka uchafu, kwa hiyo huo ndio tunaopata.

322 Angalia kipindi cha redio. Loo, jamani! Kilibadilisha *Mwamba Wenye Imara* ukawa ni kunengua. A-ha. *Msalaba Wa Kale Unaoparuza* ukawa ni kubembea, kuchezea roki. *Msalaba Wa Kale Unaoparuza,* naam, hakika, kwenye redio zetu, televisheni. Ninii yote...Walichukua hapa, si muda mrefu uliopita, shamrashamra hizo, hao wasichana wadogo. Kila kitu ni kichafu tu kama kinavyoweza kuwa, hayo ndiyo tunayopenda.

323 Yanadhaminiwa na nini? Bia, wiski, sigara, fedha za taifa. Wanafanya nini? Wanachukua pesa zao za kodi, ambazo zinapaswa kwenda kwa serikali kwa ajili ya kodi, na kulipia vipindi vichafu sana vya televisheni ambavyo wanatangaza.

324 Ilikuwa kwamba Wapentekoste wasingeenda kwenye hizo sinema chafu zenye kinyaa, wakati walipokuwa na michezo kama hiyo. Ibilisi aliwawekea moja, akaweka televisheni nyumbani mwenu.

325 Mwenendo wa nabii wa kweli ni mgumu sana, bali hebu na tudumu na ile Kweli. Naam, bwana.

326 Angalia vibao vyetu vikubwa vya matangazo. Wanawake wamesimama, sigara mkononi mwao, kila Yezebeli mdogo nchini. Nilienda kwenye . . .

327 Hivi majuzi, niliona jambo la ajabu. Kulikuwa na mwanamke mmoja aliyekuja kwenye ile shule kule, kuwachukua watoto, nilipoenda kule kuwachukua, ambaye hakuvaa kaptura; na, hiyo, hali ya hewa ni ya kuganda barafu. Kila mmoja wao akiwa na sigara. Mara walipofika kule na kusimama, endapo hawakuwa na sigara, waliiwasha upesi sana, na, "Whiu! Unaona jinsi ninavyoendelea?" Akitoa mkono huo nje ya mlango, namna *hii*, akiwa na sigara mkononi mwake. Na mtu useme jambo fulani kulihusu, loo, wanalipuka. Hakika.

328 Ukimwambia ricky ama elvis jambo fulani, ama mmoja wao huko nje, wangekupiga risasi. Na serikali ingewaunga mkono, kwa maana wao ni matineja tu. "Loo, hilo ni sawa. Wao, hawakuelewa. Wao ni matineja. Wanalipuuza."

Sasa mnaona nabii wa kweli anamaanisha nini, mwenendo wake?

329 Waangalie hawa waotaji wachafu makanisani, wakiwa na dhehebu lao, wangekupiga risasi moja kwa moja mgongoni. Jambo pekee linalowazuia kufanya hivyo, ni rehema ya Mungu, mpaka Ujumbe utakapokwisha kutolewa. Ibilisi

angekuua, kama angaliweza. Kweli. Lakini Ujumbe hauna budi kusambazwa. "Mimi Bwana nitarudisha." Hiyo ni kweli. "Ninaweza kutoka kwenye mawe haya kuuinua." Hiyo ni kweli. Vema.

330 Sinema zetu, vibao vyetu vya matangazo, wenye dhambi wetu wanaopenda anasa wakijiita Wakristo. Watu wanaojiita Wakristo; wapendao anasa, watafutao tamaa mbaya. Wanawake, waliovaa mavazi ya kizinifu; wanaume wakiwaangalia, wakiwapigia mbinja, wakijiita Wakristo, wakitoka nje. Mbona, hata wana—hata wana . . .

331 Ni jambo kubwa huko Florida, California, kwamba wana vilabu vikubwa sasa. Wanaume wote wanakusanyika na kutupa funguo zao ndani, nao wanawake wanaingia na kuchukua moja ya hizo funguo kutoka humo. Na yeyote yule awaye, anamchukua mke wake nyumbani. Wanaishi juma zima, kisha wanarudi, wanatupa ufunguo, funguo ndani tena. Unaona? Ni vilabu. Watoto waliozaliwa kiharamu na kadhalika, nguruwe akila nguruwe mwenzake, mbwa akila mbwa. Kuna nini? Ni kwa sababu wameliacha Neno.

332 Hawajui maana ya uadilifu. Huku nje wakiwa wamevaa nguo fupi, zinazobana, na vitu kama hivyo, nao wanaume wakiwatamani, nao wanafikiri kwamba ni waadilifu. Huenda hujafanya jambo lolote baya, dada, bali hebu nikwambie jambo fulani, wewe ni chombo cha ibilisi. Na kwenye Kiti cha Hukumu, BWANA ASEMA HIVI, utajibu kwa kufanya uzinzi, na nafsi yako itapotea. Unajua vyema zaidi. Unajua hilo sasa, kwa vyovyote vile. Kweli.

333 Mwelekeo wetu wote umepotoka na kuoza. Ni watu wetu, yale wanayotaka. Kama vile bwana wa nyumba, vema, kama mtu alikuwa ni bwana wa nyumba, akilaumu serikali yako . . . Hiyo ndiyo inayowatuma wavulana wetu hapa nje na kuwafanya chakula cha mzinga, kweli, kwa sababu ya upotovu wetu wenyewe. Kama tunampenda Bwana na kumtumikia Bwana, na kuipigia kura serikali nzuri na kadhalika, pangekuwa ni mahali pazuri sana. Hiyo ni kweli. Tusingekuwa na vita. La. Mungu ndiye kimbilio letu na nguvu zetu. Inawatuma wavulana wetu huko nje na kuwaua, na kuwachinja, na kadhalika, ni kwa sababu kitendo chetu wenyewe kimetimiza jambo hilo. Mungu alisema hivyo, katika Biblia, wala Yeye habadiliki. Yeye ni yeye yule tu. Ni vile watu wenu wenyewe wanavyotaka.

334 Ni kama bwana wa nyumba, vipi kama yeye ni bwana mzuri? Yeye anataka kufanya yaliyo mema. Anataka kumwishia Mungu. Naye ana familia inayopenda anasa, inayopenda maisha maovu. Mwanamume atafanya nini, wakati mkewe anataka kuvaa kaptura, na kuvaa nguo za kizinifu, na kutoka nje na kutenda kama Yezebeli, binti zake na watoto wake wote, na wote hao? Baba yake . . . Mvulana wake aliyemlea, na kumpenda, na

kumpigapiga kwa upendo na kumbusu, na kumlaza kitandani, na kumwombea, anasimama, anasema, “Mzee wangu ana kichaa. Yote anayowazia ni Biblia.” Mtu huyo atafanya nini na familia yake?

335 Ni jambo lilo hilo katika serikali yetu, kuhusu watu wake hapa. Usiilaumu serikali. Laumu kundi hili la makanisa yaliyorudi nyuma, kwa kuweka vitu kama hivyo katika siasa zao, kama walivyo navyo. Wanaipenda. Hiyo ndiyo sababu wanaipigia kura, na hiyo ndiyo sababu wanayo. Na hiyo ndiyo sababu hukumu ya Mungu iko juu yao. Nao watavuna wanachopanda. Wanapanda sasa, nao watavuna baadaye. Angalia. Loo! Tumeshikwa na wazimu. Loo, naam.

336 Tunajaribu kulipia njia yetu kuingia Urusi. Tunajaribu kulipia njia yetu na ukomunisti. Tunajaribu kulipia. Mbona, fedha, huwezi kununua karama hizi za Mungu. Kulikuwako na jamaa mmoja, Simoni, aliyejaribu kuzinunua siku moja, naye Petro akasema, “Angamia na fedha zako.” Tunacheza sehemu ya yule Simoni mchawi, kujaribu kununua karama ya Mungu.

337 Rudini kwenye Neno. Mrudieni Mungu. Rudini kwa Kristo. Ndipo msijali juu ya ukomunisti. Tutampigia kura mtu anayefaa. Tutakuwa na mtu mwingine kama Abraham Lincoln, George Washington, mtu ambaye alikuwa ni mtu halisi. Usiilaumu hiyo serikali kule juu. Tujilaumu wenyewe. Hivyo ndivyo Amosi angesema. Na hivyo ndivyo nabii yeyote wa kweli wa Mungu angesema, kama anajua Neno la Mungu. Kama yeye ni nabii wa kweli, a—anajua Neno, maana linamjia.

338 Israeli, katika mapatano yao na—na adui wao. Kwanza, iliwabidi kuliacha Neno la Mungu, kabla hawajafanya mapatano yoyote na adui wao.

339 Na kabla hatujaweza kufanya mapatano na adui zetu na kadhalika, inatubidi kuliacha Neno la Mungu. A-ha. Vivyo hivyo sasa, tunaruhusu Urumi ichukue mamlaka. Mbona, tunafanya hivyo, wakati wote. Imeichukua serikali. Inachukua mahali pengi. Imewachukua watu. Sasa inayachukua makanisa.

340 Tunafanya nini? Tumeketi kimya, tukikubaliana nao. “Loo, haileti tofauti yoyote kama ni *hivi* ama *vile*. Yote ni Mungu, kwa vyovyote.” Enyi maskini, wenye mashaka, mliorudi nyuma mnaojiita manabii. Mna shida gani? Hawajui Neno kuhusu Mungu na mambo haya. Hawalisomi Neno. Hawatambui. Wanasema ukomunisti utautawala ulimwengu. La, sivyo.

341 Urumi utautawala ulimwengu, na unafanya hivyo chini ya jina la Ukristo. Hivi Biblia, Yesu hakusema, “Itafanana sana, hata itawapumbaza walio Wateule, kama yamkini”?

342 Kile tunachohitaji leo. Hebu nifunge, katika kusema hivi. Sasa nitafunga. Tunachohitaji leo ni nabii mwingine wa kweli. Amina. Tunahitaji mtu atakayejiliwa na Neno la Mungu. Naam, ndugu. Angekataliwa na kufukuzwa, na kutupwa nje,

bali hakika angetoboa shimo. Yeye, yeye. . . Naam, A-ha. Yeye hakika angetupa Mbegu kama hizo mpaka walio Wateule wangeipata. A-ha. Hiyo ni kweli. Tunahitaji nabii. Tunamhitaji mtu ambaye hujiliwa na fasiri ya kweli ya Neno, ambaye Mungu anazungumza kupitia kwake na kulithibitisha Neno, kulifanya kweli. Hicho ndicho tunachohitaji. Na, ndugu, tumeahidiwa mmoja, kulingana na Malaki 4, "Kurudisha." Kitu gani? "Imani ya watu, irudi kwenye Biblia." Tumeahidiwa mmoja. Yeye atafanya jambo hilo.

343 Amosi alijua. Naam, bwana. Amosi alijua, Israeli, karibuni wapenzi wake wasiomcha Mungu wangewaangamiza.

344 Na wapenzi wao wa siku hizi wasiomcha Mungu watawaangamiza, kanuni zile zile za imani na kadhalika ambazo wamejifunga nazo. Enyi Wapentekoste, hicho ndicho kitu kitakachowaangamiza, kanuni zenu za imani na dhehebu. Mnajifunga wenyewe moja kwa moja huko, kuchukua alama ya mnyama, wala hata hamjui, mnayafunga macho yenu kwayo. Hakika. Ni kususiwa. Mnajaribu kufanya nini? "Wewe ni mfuasi wa *hili*, ama si mfuasi." Unaona? Hebu ngojeni tu, subirini tu, muda kidogo tu zaidi. Halafu, unasema, "Nitatoka humo wakati huo." La, hutatoka. Uko ndani yake tayari. Umetiwa alama tayari. Umeshikwa ukiwa na alama hiyo.

345 Haidhuru, Esau alilia kwa uchungu, wakati alipojua vizuri zaidi. Lakini alilia kwa uchungu, akijaribu kupata mahali pa kutubia, wala asingepapata. Utakaa humo basi. Huu ndio wakati wa kutoroka.

346 Amosi alijua ya kwamba wapenzi wao wasiomcha Mungu wangelimwangamiza, kwa kuwa wao, kanisa, lilikuwa limemwacha Yeye, Mungu na Neno Lake, njia ya Uzima. Waliiacha njia ya Mungu ya Uzima, na kufanya njia yao wenyewe. Loo, Neno lilikuwa ni jiwe la kujikwaa kwao.

347 Na ni jambo lile lile leo. Neno la Mungu ni jiwe la kujikwaa kwa wanaojiita Wakristo. Hebu mwambie kuhusu ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo. Mwambie juu ya Mungu mtakatifu. Hiyo itafanya . . .

Na, vema, wao wanasema, "Vema, tuna Roho Mtakatifu."

348 Basi kwa nini mngali mnakuwa na nywele zilizokatwa? Kwa nini mngali mnabatiza katika jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu"? Kwa nini mngali mnaamini katika mambo haya mengine ambayo mnaamini, na kutenda mnavyotenda? Inaonyesha hilo. Matunda yenu yanathibitisha jambo hilo. Yesu alisema, "Kwa matunda yao, mtawatambua." Naam. Unaona? Hiyo inaonyesha tu, unazungumza juu ya jambo usilojua kitu kulihusu. Naam, bwana. Naam.

349 Kama Amosi angalikuwa hapa, angekemea mifumo yao. Mnajua hilo?

350 Sasa nitasoma kifungu kimoja kabla ya kufunga, kifungu cha 8 cha mlango wa 3. Na hebu tusome.

> *Simba amekwisha kunguruma, ni nani asiyeogopa? Bwana. . .amenena* tayari*, ni nani awezaye neno ila kutabiri?*

351 Sikilizeni. Katika kufunga sasa, ninataka kusema hivi. Samahani kwa kuwacheleweshа, tumechelewa kwa muda wa nusu saa. Lakini, angalieni. Ninataka kusema hivi. Mimi ni mwindaji. Mimi huwinda. Ninashukuru Mungu alinipa kitu kama hicho.

352 Hivi majuzi wakati bunduki ilipolipuka, nilishuka nikaenda moja kwa moja kule chini, nione kama ningeweza kulenga shabaha tena. Sitaki hilo liniogopeshe. Kama ningalipata ajali, huko barabarani, nisingeacha kuendesha gari. Kama nikitembea sakafuni na kujikwaa kidole changu kwenye zulia, na nikapitia dirishani, nisingeacha kutembea. Unaona? La, la. Mungu alinipa mazoea safi. Huyo alikuwa ni Shetani. Huyo hakuwa ni Mungu. Unaona? Huyo alikuwa ni Shetani.

353 Sasa, ninajua matumizi ya kiroho ya jambo hilo. Tuko watatu humu chumbani sasa hivi, wanaojua kwamba ni kitu gani. Na lingesimamisha nywele kichwani mwako, bali nisingemwambia mtu yeyote. Unaona? Ni watu hawa watatu tu, kwa ajili ya thibitisho. Sasa, yote ni sawa. Yote ni. . .Mungu alijua yote kuhusu hilo, na alilionya mbele, na kadhalika. Nasi tunajua hilo. Kwa sehemu ilikuwa ni kosa langu, nami nilikuwa na kitu fulani.

354 Ni—nilimtetea mtu mmoja siku moja, wakati haikunipasa kumtetea. Ningalimshtusha nusura afe. Unaona? Badala ya kufanya hivyo, ilinibidi kulipia hilo. Kwa hiyo, basi, kwa hiyo sisi. . .Hilo ni sawa. Ni mimi, na limesamehewa sasa. Nasi tutaendelea. Unaona? Naam.

Amosi, kifungu hiki cha 8, “Kama simba akinguruma, ni nani asiogope?”

355 Nimewinda kwenye misitu ya Afrika. Nimekuwa mahali ambapo simba walikuwa. Yeye ni mfalme wa wanyama. Nimelala misituni usiku na kusikia vilio vya maumivu na fisi, kule kucheka na mlio mkali, na—na ninii—na wanyama mbalimbali. Halafu baadhi ya hao fisi wangefanya, ingegandisha damu yako wakati wanapolia. Na kule pamoja na chui, na mlio wa farasi, na kadhalika, na mende, na tumbili, na nyani, na maelfu mara maelfu, “vilio vyembamba vya maumivu.” Ukitembea kila mahali, unaweza kusikia kila namna ya vitu vikiendelea. Bali hebu simba angurume, mende hata watanyamaza kimya. Ni unyamavu wa kutisha. Wao hutulia. Kwa nini? Mfalme wao amenena. Amina.

356 “Kama simba akinguruma, ni nani asiyeogopa? Mungu anaponena, ni nani awezaye neno ila kutabiri?” Mungu

anaponena, nabii hupaza sauti. Mnajua ninalomaanisha? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Nabii wa kweli hulia. Marafiki, Yeye amenena. Basi, hebu kila kiumbe cha Ufalme Wake kisikilize yale aliyosema.

357 Kama simba anaweza kutambua ya kwamba kuna kasoro fulani, wakati anaponguruma, kila kitu cha ufalme wake hunyamaza. Wanasikiliza. Hata mende wadogo, hata hivyo, yeye yuko katika ufalme wa simba huyo. Kilio hicho kikali sana cha fisi, yeye hufunga domo. Huyo ndovu pale, anayeweza kumnyanyua huyo simba, na kumzungusha-zungusha kwa ninii yake, "Wiiil! Wiiil!" Na hebu simba angurume, yeye atafunga domo na kusimama kimya. Hebu nyati wa rasi, ambaye anaweza kukoroma, ionekane kama ni moto uliopuliziwa puani mwake. Wakati simba akimrukia, hata hawezi kumdhuru. Hebu kifaru, akiwa na silaha zake za tani saba, amchome, na pua yake kubwa. Hebu simba angurume, anasimama mahali alipo. Kuna nini? Mfalme wake amenena. Unaona? Anataka kusikia yatakayosemwa.

358 Na wakati Mungu anaponena, nabii hupaza sauti. Basi hebu na Ufalme Wake usikie yale anayosema. Mungu amenena. Hebu kila kiumbe cha Ufalme Wake kisikilize yale anayosema.

Na tuombe.

359 Ee Simba, wa kabila la Yuda, simama na ungurume! Wewe unanguruma katika siku hii ya mwisho. Macho yako yamefinyaa. Unaangalia chini. Unaona dhambi za taifa hili na ulimwengu unaojiita wa Kikristo. Unaona dhambi ya taifa hili, wakati limenunuliwa kwa Damu ya thamani. Unaona jinsi madhehebu yanavyogaagaa juu ya Neno Lako. Unaona jinsi manabii wa uongo wanavyosema uongo. Wanaukana Ukweli wa Mungu.

360 Nguruma, Ee Simba wa Yuda! Jalia manabii wako wapaze sauti. "Mungu anaponena, ni nani awezaye neno ila kutabiri?" Ni Neno la Mungu likitoka katika Biblia, likipitia kwa nabii. Anawezaje kutulia? Kama angetulia, angepasuka vipande-vipande. Ee Mungu, jalia nabii Wako angurume, Bwana. Nguruma Ujumbe Wako, Mungu, na jalia kila kiumbe cha Ufalme Wako kisikilize.

361 Jalia wakome. Jalia wanawake wasimame na kujichunguza wenyewe. Jalia wanaume wasimame na wajichunguze wenyewe. Jalia kila mhubiri anayesikiliza kanda hii, asimame na kujichunguza mwenyewe, kwa maana Simba wa kabila la Yuda ananguruma. Na Neno la kweli linawajia manabii, wanene, waseme kwa sauti kuu, "Tubuni mkageuke kabla ya kuchelewa sana."

362 Mungu, ninaukabidhi Ujumbe huu, kwenye kanda na wasikilizaji hawa wanaoonekana, Kwako asubuhi ya leo, nikitumaini utaukubali. Na umwite kila mwana na binti wa Mungu, aliye chini ya...atakayepata kusikia kanda hii,

ama chini ya mlio wa sauti, watarudi wakatubu kabla ya kuchelewa sana.

363 Nami ninaamini, Bwana, kama ungemtuma Amosi hapa, angepalizia sauti jambo lilo hilo. Kwa maana asingeweza kupalizia sauti . . . Lakini kama yeye ni nabii wa Bwana, yeye ni mtangazaji wa Neno. Yeye ametumwa na Neno, pamoja na Neno, naye ni Neno. Sasa, Bwana, jalia itendeke, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mwenendo Wa Nabii Wa Kweli Wa Mungu SWA62-0513M
(The Way Of A True Prophet Of God)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 13 Mei, 1962, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org